**MAKABURI** ya watu 88 waliofariki ajali ya treni yageuzwa maficho ya vibaka

UKURASA 8

**FAMILIA** zalala nje dalali wa korti akifunga nyumba zao

UKURASA 15



**MALEZI**, makuzi mabovu chanzo ongezeko la VVU kwa vijana nchini

UKURASA 16


# Nipashe

Jumatatu Machi 18, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581619

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@nipashe.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**REAL MADRID SASA YAMBANIA MBAPPE**

UKURASA 22

## KIFO CHA JPM

# Jenerali Mabeyo aanika ilivyokuwa



Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali Venance Mabeyo

**ATAJA** hatua tatu nzito zilizomwelemea, mvutano wa vigogo hadi kumwapisha Samia... Endelea Uk. 2



## Bashe atoa ufafanuzi mchele wa Marekani kuletwa nchini

UKURASA 19

## Bei ya vyakula yauma, yapuliza katika mfungo

UKURASA 4




MIAKA 3 YA UBORA



Mhe. **Dr. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya M uungano wa Tanzania

**Salamu za Pongezi**

Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa **Bharya Engineering and Contracting Company Limited** , tunaungana na Watanzania wote **kupongeza Rais** wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kut**imiza miaka mitatu ya ubora ofisini kwa utendaji na uwajibikaji wake katika kusimamia na kutekeleza y**ale aliyoya**ahidi ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu.
Pia tungependa kumshukuru MH. Mama wa Taifa kwa kufungua milango ya biashara kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kujenga mahusiano bora kwenye biashara na amani.
Tunamuombea afya njema na tuko pamoja katika kuhakikisha agenda ya maendeleo ya Watanzania inafanikiwa.

TUNAKUTAKIA KILA LA HERI KWENYE MIAKA IJAYO !

RAMADAN KAREEM!

BECCO


**MICHEZO** **CHAMA: AL AHLY WETU, JOB ATOA SIRI YANGA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

KIFO CHA JPM

# Jenerali Mabeyo aanika ilivyokuwa

Christina Mwakangale na Beatrice Audax

MKUU wa Majeshi mstaafu, Jenerali Venance Mabeyo, amezielezea saa ngumu za maagizo alizozipitia wakati Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli alipozidiwa hospitalini hadi kufariki dunia.

Jenerali Mabeyo amesema ameweka wazi maagizo mawili aliyopewa na Rais Magufuli alipobaini alikuwa anakaribia kufariki dunia; kwanza aliagiza aondolewe Hospitali ya Mzena, iliyoko Makumbusho, Dar es Salaam, ambako alilazwa na arudishwe nyumbani.

Mkuu huyo wa Majeshi mstaafu amebainisha agizo la pili lilikuwa kutoa wito kwa viongozi wa dini, akiwamo Paroko wa Kanisa alilokuwa anaabudu (Hayati Magufuli) pamoja na Kardinali Polycarp Pengo.

"Aliniita 'CDF (Mkuu wa Majeshi) njoo, akaniambia siwezi kupona, waamuru hao madaktari waniruhusu nirudi nyumbani'. Nikamwambia 'Mheshimiwa, sina mamlaka hayo'. Akasema 'yaani CDF unashindwa kuwaamuru wanirudishe nyumbani!'.

"Nikamwambia 'suala la afya, si la CDF, Mheshimiwa, ninaomba ubaki utulie, madaktari watatuambia'. Siku hiyo hiyo alipoona nina msimamo huo, akaniambia niitieni paroko wangu, Paroko wa Oysterbay (St. Peters), Makubi," amesema Mkuu wa Majeshi mstaafu.

Jenerali Mabeyo aliyasema hayo katika mazungunmzo na chombo cha habari cha serikali cha mtandaoni (Daily News Digital), akisema wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini, akiwamo yeye, walifika kumwona Rais Magufuli mara tatu kila siku chini ya uangalizi wa Prof. Mohamed Janabi, wakati huo akiwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema Hayati Magufuli aliagiza waitwe viongozi hao wa dini saa chache kabla ya hali yake kubadilika. Viongozi hao walipofika, walimsalia ibada ya sakramenti ya upako wa magonjwa kwa aliyekuwa na hatari ya kifo.

"Asubuhi yake, aliagiza waitwe paroko wake na Kardinali Pengo, walipofika kwa taratibu za kikatoliki, walimsalia sakramenti ya upako wa magonjwa kwa aliyekuwa na hatari ya kufariki (dunia). Ilipofika mchana wakanipigia simu watu wa hospitalini.

"Wakampigia DGIS (Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa), mimi (Mabeyo), IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi), 'hali ya mheshimiwa si nzuri sana'. Tukamkuta ametulia, lakini alikuwa hawezi kuongea tena, tukawaita madaktari wengine, Prof. Lawrence Museru na Prof. Mohamed Janabi alikuwapo pale muda wote, wakijaribu kumhudumia, tulikaa hadi jioni, ilipofika saa 12 na nusu au moja kasoro, alifariki (dunia)," alisema Mabeyo.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Biteko (kushoto), akitoa heshima katika kaburi la Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli baada ya Misa Takatifu ya kumwombea Rais huyo iliyofanyika katika Kanisa Katoliki, Parokia ya Mt. Yohana Maria Muzeyi, wilayani Chato mkoani Geita jana. Kushoto kwake ni Mjane wa Hayati Magufuli, Janeth Magufuli. Kulia ni Mbunge wa Chato, Dk. Medard Kalemani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Baada ya madaktari kuthibitisha kifo cha Dk. Magufuli, Jenerali Mabeyo alitaja ulikuwa wakati mwingine mgumu kwake; namna ya kutoa taarifa, kwa familia yake, kwa viongozi wakuu wa nchi akiwamo Makamu wa Rais (wakati huo Samia Suluhu Hassan) akiwa ziarani mkoani Tanga.

"Makamu wa Rais wakati huo hayupo Dar es Salaam, Katibu Mkuu Kiongozi hakuwapo Dar es Salaam, tulikuwapo sisi tu watatu. Tukasema kwa kuwa Makamu wa Rais yuko Tanga, ngoja tumwambie Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi waje, bila ku-disclose (kufichua).

"Wakaja mapema, mimi kama mwenyekiti wa wakuu wa vyombo, nilitakiwa kufichua, Mheshimiwa Rais ameshatutoka. Tukaanza kushauriana, tufanyeje? Nani anatakiwa kutangaza kwenye vyombo vya habari wananchi wajue?" Jenerali Mabeyo alisimulia.

Katika hilo, Jenerali Mabeyo alisema iliwapasa kurejea kwenye Katiba ili wathibitishe kisheria, ikizingatiwa suala hilo halikuwa na uzoefu nchini - Rais kufariki dunia akiwa madarakani.

"Tukaanza kutafuta Katiba kwanza inasema nini? Mtu pekee anayeweza kutangaza kwenye vyombo vya habari ni Makamu wa Rais, na yeye yuko Tanga. Tunampigia simu au tunamwambia aje? Yakafanyika mawasiliano mengine kumwambia aje.

"Lakini kabla ya kutangaza, tukasema familia (ya Dk. Magufuli) yake haijui. Mke wake yupo hapa Ikulu. Mama yake (Mama wa Dk. Magufuli) anaumwa, yuko Chato (Geita), hajaambiwa, hatuwezi kumwambia kwa simu, nani anayekwenda kumwambia mke wake? Na mwingine wa kwenda Chato? Tukatafuta ndege 'charter'," alisimulia.

Jenerali Mabeyo alisema hatua hizo zote zilichukua ndani ya takribani saa tano, ikiwamo kuwaita Dar es Salaam viongozi kadhaa akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pamoja na kutoa taarifa kwa familia ya Dk. Magufuli na mama yake aliyekuwa Chato, ndipo kifo chake kikatangazwa rasmi katika vyombo vya habari saa tano usiku (tarehe kama ya jana mwaka 2021).

Kiongozi huyo wa jeshi pia aliweka wazi kwamba kumwapisha Rais mpya lilikuwa jambo lingine gumu kwao. Alisema kulikuwa na mawazo ya aina mbili; aapishwe Rais mpya kabla au baada ya maziko.

"Suala lilikuwa Rais aapishwe kabla ya kuzika au aapishwe baada ya kuzika.

Tukasema kuna marais watakuja kutoka nje kuja kumzika mwenzao, watapokewa na Rais au Makamu wa Rais? Lazima awapo mwenzao (Rais), ndio maana tukafikia uamuzi Makamu wa Rais aapishwe kuwa Rais.

"Ndio maana zilipita siku mbili, kikatiba haitakiwi. Katiba inaelekeza ni ndani ya saa 24 awe ameshatangazwa Rais. Tarehe 17 na 18, ikapita na 19 (Machi 2021) ndipo akatangazwa Rais.

"Kulikuwa na majadiliano hapo... tunashukuru Mungu... namna ya kumwapisha kulikuwa na mjadala pia.

Wengine wakasema isiwe ni sherehe, wengine iwapo sherehe, sasa nilichosema, lazima gwaride liwapo, bendera ya Amiri Jeshi Mkuu lazima ipande. Kulikuwa na mvutano... 'tuko kwenye msiba hakuna gwaride', nikasema huyu ni Amiri Jeshi Mkuu anayeapishwa, asipoapishwa kwa taratibu za kitaifa, jeshi halitamtambua," alisimulia.

Mkuu wa Majeshi mstaafu alisema mjadala mwingine ulikuwapo katika jinsi, kwamba Amiri Jeshi Mkuu aitwe kwa jina gani, kuwatambulisha.

"Sisi katika jeshi hatuwatambui wanawake na wanaume, ndio maana jeshini tuna ofisa na askari, hakuna mwanamume na mwanamke, hata Amiri Jeshi litabaki kuwa hivyo, ni 'commanding chief'. Amirat ni kiongozi wa dini kwa nchi zinazoongozwa kidini. Tuliwashirikisha pia BAKITA," Jenerali Mabeyo alisema.

Aliongeza kuwa Rais Magufuli alimteua Makamu wa Rais, akiwa msaidizi wake katika kipindi chote kwenye mamlaka akifuatwa na Waziri Mkuu.

"Rais Samia ameingia madarakani kwa tukio... tunamshukuru Mungu, mpito ulikwenda vizuri. Kwa mujibu wa Katiba, imeelezwa endapo Rais atafariki, au atashindwa kutekeleza majukumu yake kama Rais, atakayeshika madaraka ni Makamu wa Rais.

"Inawezekana watu... Katiba wakawa wameisahau kidogo... ni Rais mzuri kwa sababu anawashirikisha watu, mara nyingine wanaomshauri wanakosea, lakini anashirikisha taasisi, kitaaluma," alisema Jenerali Mabeyo.

Kifo cha Rais Magufuli kilitangazwa usiku na Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan Machi 17, mwaka huu, akieleza kuwa kilitokana na maradhi ya moyo yaliyokuwa yanamsumbua kwa muda mrefu. Siku mbili baadaye, Samia aliapishwa kuwa Rais kwa mujibu wa Katiba ya nchi, toleo la 1977.

**KUMKUMBUKA JPM**

Katika ibada maalum ya kumwombea Hayati Maguful, Makamu Askofu wa Jimbo Katoliki la Rulenge Ngara, Padri Ovan Mwenge iliyofanyika katika Parokia ya Mtakatifu Yohana Maria Muzeyi Mlimani, Jimbo Katoliki la Rulenge Ngara, wilayani Chato mkoani Geita, alikumbusha jamii kuendelea kumwombea mara kwa mara na kuacha kuhukumu pale alipokosea kama binadamu.

"Kama alikuwa na upungufu, Mungu amsamehe na kumkaribisha katika ufalme wa mbinguni maana huenda yeye kama binadamu kuna mahali alikosea," alisema Padri Mwenge wakati akiongoza ibada hiyo.

Alisema waamini Katoliki na Watanzania kwa ujumla wataendelea kumkumbuka kwa kazi alizolifanyia taifa kwa nyakati tofauti na wala si kazi ya binadamu kuhukumu, bali ni kumwombea, kama kuna watu hawaamini katika kumwombea marehemu, wabaki hivyo hivyo na kama kuna watu wanaamini wafanye hivyo.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko aliyeshiriki ibada hiyo, akimwakilisha Rais Samia, alisema maono yote ya Hayati Magufuli yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Alisema Hayati Dk. Magufuli alikuwa na ndoto ya kuunganisha Watanzania kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo na sasa Rais Samia anaendeleza miradi hiyo.

"Rais Samia ameendeleza ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwl. Julius Nyerere, reli ya kisasa ambayo majaribio yamefanyika kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro pamoja na ujenzi wa Daraja la Kigongo- Busisi ambalo limefikia asilimia 85 likiunganisha mikoa ya Geita na Mwanza, ninataka niwahakikishie hakuna kitakachosimama," alisema Dk. Biteko.

Alisema kauli ya Rais Samia ya Kazi Iendelee alikusudia kuyaendeleza yale yote yaliyobuniwa na Hayati Dk. Magufuli na kuwahakikishia kwamba yote aliyoyaanzisha Rais Dk. Magufuli anayaendeleza kwa kasi kubwa ili Watanzania wayapate kama walivyoyakusudia kwa Hayati Dk. Magufuli.

**MTOTO WA JPM**

Akiwasilisha salamu za familia, Mtoto wa Hayati Dk. Magufuli, Jesca Magufuli alisema watamkumbuka kwa kupenda maendeleo na kutanguliza mbele maslahi ya nchi.

Mjane wa Hayati Dk. Magufuli, Janeth Magufuli alishukuru viongozi wa dini na serikali kwa jinsi wanavyoshirikiana na familia hiyo katika kuyaenzi yote ambayo alikusudia kuyatenda.

Ibada hiyo iliambatana na kumbukizi ya miaka mitatu tangu kifo cha Hayati Dk. Magufuli kilichotokea Machi 17, 2021, iliyofanyika nyumbani kwake na kuhudhuriwa na wanafamilia wakiongozwa na Janeth Magufuli, wananchi, viongozi wa dini na serikali akiwamo Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella

## MATANGAZO


# NOTICE OF SALE AND INVITATION OF SEALED BIDS FOR SALE OF PROPERTY

LEGENDS AUCTION MART GENERAL BROKER LIMITED

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT under the powers contained in the law and Mortgage Deed and other powers enabling us to do so, We LEGENDS AUCTION MART LIMITED of P. O. Box 80310, Dar es Salaam, duly appointed by the AKIBA COMMERCIAL BANK PLC (the 'Bank') to sell the mortgaged property "as is" by sealed bids; DO HEREBY INVITE BIDS FROM THE GENERAL PUBLIC for the outright purchase of the property described in the table below;

| Property Description | Location | Bids Submission Date | Bids Opening Date | Minimum Bids Price |
|---|---|---|---|---|
| Farm with sales agreements (194 acres ) | Tomoni Village-Kibiti Rufiji | On 26th March 2024 before 10:00 Hours at the address below. | On 28th March 2024 at 10:30 Hours at the address below. | TZS 600,000,000/= |





TERMS AND CONDITIONS:

1. Bid must be submitted in sealed envelope clearly marked "BID FOR THE PURCHASE OF TOMONI PROPERTY - LEG/TOM/01/2024", including full address of the bidder.
2. The successful Bidder shall be required to deposit 25% of the bid price within 24 hours from the date/time of the award and balance 75% of the bid price within 14 days from the date of the award or within such other time as we may prescribe; failure of which the offer shall be revoked forthwith and the 25% down payment shall be forfeited and the next highest bidder who meets the conditions may be awarded, or cancel the sale process altogether.
3. Bids must be submitted and shall be opened on the date and address described herein. Bidders are invited to attend opening ceremony event if they so wish.
4. The property is being sold on "AS IS" basis, the Bank and us shall have no further liability after the sale.
5. The interested parties will be allowed to inspect the property by prior appointment.
6. All the information contained in this advertisement is free from liability.
7. The successful bidder or otherwise shall be notified within a maximum of five [5] working days after bid opening; either to his/her physical address or his/her email address, which shall be sufficient communication.
8. The Bank and we shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all or reject any or all the bids without having to assign any reasons.
9. All costs regarding transfer of ownership shall be borne by the successful bidder.
10. All bids shall be addressed to the address below.

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
P.O.BOX 669,
Amani Place, 3th Floor
Posta, Dar es Salaam, Tanzania.
+255 (0) 768790476

# NOTICE OF SALE AND INVITATION OF SEALED BIDS FOR SALE OF PROPERTIES

MAJEMBE AUCTION MART LIMITED — HAKI NA KAZI

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT under the powers contained in the law and Mortgage Deed and other powers enabling us to do so, We MAJEMBE AUCTION MART LIMITED of P. O. Box 70708, Dar es Salaam, duly appointed by the AKIBA COMMERCIAL BANK PLC (the 'Bank') to sell the mortgaged property "as is" by sealed bids; DO HEREBY INVITE BIDS FROM THE GENERAL PUBLIC for the outright purchase of the property described in the table below;

| Property Description | Location | Bids Submission Date | Bids Opening Date | Minimum Bids Price |
|---|---|---|---|---|
| Property with CT. No.DS-MT1001536 | Madale- Kinondoni | On 26th March 2024 before 10:00 Hours at the address below. | On 28th March 2024 at 10:30 Hours at the address below. | TZS 596,000,000/= |

TERMS AND CONDITIONS:

1. Bid must be submitted in sealed envelope clearly marked "(1) BID FOR THE PURCHASE OF MADALE PROPERTY - MAJ/MDL/02/2024", including full address of the bidder''
2. The successful Bidder shall be required to deposit 25% of the bid price within 24 hours from the date/time of the award and balance 75% of the bid price within 14 days from the date of the award or within such other time as we may prescribe; failure of which the offer shall be revoked forthwith and the 25% down payment shall be forfeited and the next highest bidder who meets the conditions may be awarded, or cancel the sale process altogether.
3. Bids must be submitted and shall be opened on the date and address described herein. Bidders are invited to attend opening ceremony event if they so wish.
4. The property is being sold on "AS IS" basis, the Bank and us shall have no further liability after the sale.
5. The interested parties will be allowed to inspect the property by prior appointment.



6. All the information contained in this advertisement is free from liability.
7. The successful bidder or otherwise shall be notified within a maximum of five [5] working days after bid opening; either to his/her physical address or his/her email address, which shall be sufficient communication.
8. The Bank and we shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all or reject any or all the bids without having to assign any reasons.
9. All costs regarding transfer of ownership shall be borne by the successful bidder.
10. All bids shall be addressed to the address below.

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
P.O.BOX 669,
Amani Place, 3th Floor
Posta, Dar es Salaam, Tanzania.
+255 (0) 768790476

# Bei ya vyakula yauma na kupuliza

Na Waandishi Wetu




BEI za bidhaa za vyakula imeendelea kupaa katika maeneo mbalimbali nchini huku Dar es Salaam ikiwa juu zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine, lakini baadhi sehemu ikishuka.

Vitunguu havishikiki katika masoko mengi kutoka na kupanda kwa kasi kwa kipimo maarufu cha 'Sado' ndogo kuuzwa hadi Sh. 10,000.

Bei elekezi ya sukari iliyowekwa na serikali haifuatwi na baadhi ya wafanyabiashara hali iliyosababisha watu 40 kukamatwa kwa kosa hilo visiwani Zanzibar.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini katika maeneo tofauti vyakula vinavyotumika kwa wingi katika kipindi cha mfungo wa Kwaresima na mwezi wa Ramadhani, vimepanda madaradufu.

Fungu moja la magimbi sasa linauzwa Sh. 3,000 badala ya Sh. 2,000 na mihogo fungu linauzwa Sh. 2,000 badala ya Sh. 1,000 katika mnada wa vyakula eneo la Boko Maliasili.

Masoko ya Dar es Salaam, likiwamo la Tandika, bei ya nyanya imepanda kutoka Sh. 5,000 kwa sado hadi Sh. 7,000; vitunguu swaumu kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 8,000.

Mboga za majani fungu moja linauzwa kati ya Sh. 700 na 1,000 kutoka bei iliyozoeleka ya Sh. 500 na kabichi ndogo inauzwa Sh. 1,500 kutoka Sh. 500 na 700 huku kubwa ikiuzwa hadi Sh. 4,000.

Nipashe imebaini pia baadhi ya maeneo sukari imeshuka kutoka Sh. 4,500 na 5,000 kwa kilo hadi Sh. 3,600.

Katika baadhi ya maduka yaliyokuwa yanauza kwa Sh. 4,500 mapema mwezi huu sasa wanauza Sh. 4,000 hadi Sh. 3,600. Unga wa sembe katika baadhi ya maduka makubwa Kata ya Toangoma, Manispaa ya Temeke, unauzwa kilo 10 Sh. 12,000 badala ya Sh. 13,000, huku kwenye masoko madogo katika eneo hilo, vitunguu sado moja ni Sh. 9,000 hadi Sh. 10,000 wakati ndoo ndogo ya viazi mviringo ikipanda hadi Sh. 14,000 kutoka Sh. 12,000.

Katika Soko la Tegeta kwa Ndevu, sado moja la nyanya inauzwa Sh. 9,000 kutoka 5,000 au 4,000 ya awali, huku kitunguu kimoja kinauzwa Sh. 200 na nyanya moja Sh. 150 mpaka Sh. 200.

Fungu la viazi vitamu na mihogo lililokuwa linauzwa kwa Sh. 1,000 katika soko hilo sasa linauzwa Sh. 2,000, tambi za kupima, kilo moja Sh. 2,900 na maharagwe kilo moja ni kuanzia Sh. 3,000 mpaka 3,500, kilo ya nyama Sh. 9,000 kwa soko hilo la Tegeta na mchele ni kuanzia Sh. 2,000 hadi 3,500.

Baadhi ya wafanyabiashara walioongea na Nipashe walisema wamelazimika kupandisha bei kwa sababu wananunua kwa bei kubwa katika eneo wanakozitoa.

Katika eneo la Mbezi Luizi, Malamba Mawili na Msigani, wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam, maharagwe yanauzwa kilo Sh. 2,500 hadi 3,000, mchele 2,400 hadi 3,200 huku sukari ikiuzwa Sh. 3,800, tambi 2,200 na mafuta ya kula ya kupima lita moja Sh. 3,800, galoni la lita tano la alizeti Sh. 28,000 na ngano kilo moja Sh. 2,800.

## DODOMA

Soko Kuu la Majengo na Sabasaba bidhaa zinazotumika kwenye mfungo zimeongezeka bei huku sukari ikiendelea kuwa juu.

Kilo moja ya sukari inauzwa kati ya Sh. 2,900 hadi 4,000 kwa kilo, mafuta ya kula lita ni Sh. 5,000, bei ya mchele ni kati ya Sh. 2,600 hadi 3500, magimbi fungu Sh.1,000 hadi 2,000, mihogo Sh. 500 hadi 2,500.

## ZANZIBAR

Kabla ya mfungo wa Ramadhani serikali iliwataka wafanyabiashara kutopandisha bei za bidhaa ili kutoa unafuu kwa wananchi hasa wanyonge kumudu gharama na kununua vyakula kwa ajili ya futari, lakini ombi hilo limeonekana kupuuzwa na baadhi ya wafanyabiashara.

Nipashe imebaini masoko mbalimbali likiwamo la Darajani, Mwanakwerekwe na Jumbi nyanya kilo moja inauzwa Sh. 3,000 badala ya Sh. 2000, vitunguu maji kilo moja Sh. 4,500 badala ya Sh. 3,000, maharagwe kilo 3,500 na badala ya 2,800.

Fatma Jabu mkazi wa Mjini Unguja, aliomba serikali inapotoa agizo lifanyiwe kazi ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi hasa katika mwezi huu wa Ramadhani ambao unamahitaji mengi.

Mkurugenzi wa Tume ya Ushindani Zanizabar, Muhammed Sijiamini Muhammed, alisema hadi jana wameshawakamata wafanyabiashara zaidi ya 40 kwa kuuza sukari kinyume na bei elekezi iliyotolewa na serikali.

"Katika operesheni yetu tumegundua kuwa kuna wafanyabiashara wadanganyifu wanauza sukari kinyume na bei elekezi ya serikali na unapowauliza hujifanya wanauza bei halali kumbe ni kinyume ya hapo na tayari maduka zaidi ya 40 tumeyafungia," alisema.

## KANDA YA ZIWA

Mfanyabiashara Neyemia Sancho, alisema bei ni ya kawaida kutokana na wingi wa bidhaa sokoni.

Mwenyekiti wa Soko Kuu Manispaa ya Shinyanga, Alex Stephen, alisema baadhi ya watu wameshaanza kuvuna mazao hali inayofanya baadhi ya bei za bidhaa kushuka na kutoa mfano wa kilo ya mchele iliyokuwa ikiuzwa Sh. 2,400 hadi 5,000 sasa ni Sh. 1,900 hadi 2,000.

Alisema unga wa ugali uliokuwa ukiuzwa Sh. 1,300, sasa ni Sh. 1,100, huku akibainisha kwamba licha ya bidhaa kushuka bei, lakini mzunguko wa biashara sio mkubwa kutokana na dini zote mbili kuwa kwenye mfungo.

Kuhusu sukari ambayo inatumika zaidi katika maandalizi ya futari kwa waumini wa kiislamu, mfanyabiashara wa duka la rejareja, Bahati Patrick, alisema bado haijashuka, bei ni Sh. 3,200 kwa kilo, kutokana na upatikanaji wake kuwa mgumu.

Bei elekezi ya sukari ambayo ilitolewa na serikali kwa upande wa Kanda ya Ziwa kilo moja iuzwe Sh. 2,800 hadi 3,000.

Mkazi wa Majengo wilayani Kahama, Aisha Juma, alisema awali walikuwa wakinunua maharage kilo moja kwa Sh. 2,000 mpaka 2,200 sasa wananunua Sh. 1,500 mpaka 1,700 kwa baadhi ya maeneo.

Alisema mchele waliokuwa wakiununua kilo moja kwa Sh. 2,200 hadi 2,800 sasa hivi umeshuka hadi Sh.1,700 huku lita moja na nusu ya mafuta ikiuzwa kwa Sh. 5,500 hadi 6,000 kutoka bei ya awali ya Sh. 7,000.

## TANGA

"Hali ya kiuchumi imekuwa ngumu sana bila kujali wenzetu wafanyabiashara wanapandisha futari bei, kuna siku mtu unakosa hata pesa ya kununua sukari, kwa sasa sukari inauzwa kilo Sh. 4,600 hadi 5,000, na kila siku bei zinabadilika hakuna bei elekezi iliyofanyiwa kazi," alisema Hamza Nassoro.

"Ukienda sokoni magimbi hayashikiki, kabla ya mwezi Ramadhani Sh. 1,000 unapata magimbi, lakini kwasasa ni kuanzia 3,000 tena yanapangwa mawili au matatu, nazi tunanunua hadi Sh. 1,700, hii hali ni ngumu sana, tunaomba serikali iweke bei maalumu ambayo itakuwa nafuu kwetu kuweza kujikimu katika kipindi hiki kigumu," alisema.

## TAKWIMU ZA NBS

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, fahirisi za bei za taifa kati ya mwezi Januari, 2024 na Februari, 2024 zimeongezeka kwa asilimia 0.5 na ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula.

# 'Msitu wa Pugu Kazimzumbwi utangazwe'

Na Elizabeth Zaya

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeelekeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuongeza nguvu ya kutangaza vivutio vya utalii katika Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi ulioko Kisarawe, mkoani Pwani.

Wajumbe wa kamati hiyo walielekeza hayo mwishoni mwa wiki walipotembela hifadhi ya msitu huo kwa lengo la kuona miradi mbalimbali inayotekelezwa na TFS ikiwamo iliyotokana na fedha za kukabili athari za UVIKO-19.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Murtaza Giga, alisema TFS imefanya kazi kubwa kutengeneza miundombinu na kulinda msitu huo, akiagiza nguvu zaidi iongezwe, hasa katika kutafuta fedha za ndani na kwa wadau mbalimbali zisaidie kutangaza na kufanya maboresho zaidi ya miundombinu.

"Sisi kama kamati ambayo tunasimamia sekta hii, kwa kiasi kikubwa tumeridhika vya kutosha kwa namna fedha za UVIKO-19 zilivyotumika kwenye miradi ndani ya msitu huu.

"Kazi iliyofanyika kupitia fedha hizi inaonekana na vinaendana, nisema tu kwamba ushirikiano tunaofanya kati ya wizara hii na kamati una matokeo mazuri.

"Wajumbe mbalimbali wameshauri kwamba pamoja na kazi kubwa ambayo imefanyika, wameona pia kuongeza nguvu zaidi kwenye kutangaza hifadhi hizo na kuwekeza zaidi kwenye maboresho ya miundombinu kuendana na ongezeko la watalii wanaokuja," alielekeza.

Waziri wa Maliasili na Utali, Angellah Kairuki, alisema wanaendelea kuboresha miundombinu ya hifadhi ya msitu huo na mingine pamoja na kutangaza vivutio vilivyopo.

Angellah alisema wanaandaa mpango wa uwekezaji utakaowawezesha kufahamu namna ya kuwekeza katika hifadhi ya msitu huo wa Pugu Kazimzumbwi.

Kamishna wa Uhifadhi Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alialika wawekezaji kuwekeza katika eneo lolote kwenye hifadhi ya msitu huo kwa ajili ya kutoa huduma za utalii.

"Tumebaini kwamba baada ya kutekeleza miradi hii, kumekuwa na ongezeko kubwa la watalii wanaokuja kutembelea, hata wabunge wameliona hilo, wakatushauri tuchukue hatua mahususi kutangaza zaidi vivutio hivi na kuongeza jitihada za kutafuta fedha zetu za ndani na kwa wahisani ili tuboreshe zaidi miundombinu kuhimili ongezeko hili la watalii," alisema Prof. Silayo.

"Kwa sababu tunaamini wapo wawekezaji wengi wenye weledi na jukumu hili wanaweza kulitekeleza vizuri zaidi na kutoa huduma za kimkakati, tunawaalika waje kuwekeza," alisema.

Prof. Silayo alibainisha kuwa idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi za misitu imeongezeka kutoka wageni 96,000 miaka mitatu iliyopita hadi kufikia 242,000 kwa mwaka sawa na ongezeko la asilimia 117,000 huku mapato yakiongezeka kutoka Sh. milioni 333 hadi Sh. bilioni 1.5 kutokana na huduma za utalii pekee katika misitu hiyo.

TFS ilianzishwa kisheria kupitia Tangazo la Serikali (GN 269) la Julai 30, 2010 na kuzinduliwa rasmi tarehe Julai 18, 2011 kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti na wenye ufanisi na tija wa rasilimali za misitu na nyuki; kuongeza ubora na thamani ya kifedha katika kutoa huduma kwa umma; na kuendelea kukuza na kuboresha uwezo wa kutoa huduma kwa umma.

TANGAZO


SALEHBHAI
GLASS INDUSTRIES LTD
GLASS TOUGHENERS, PROCESSORS
AND GLAZING CONTRACTOR
HONGERA
MHE. DKT SAMIA
SULUHU HASSAN
KWA KUTIMIZA MIAKA
MITATU
MADARAKANI
2021 - 2024
Bodi ya Wakurungenzi, Menejimenti na
Wafanyakazi Wote wa SALEHBHAI GLASS INDUSTRIES LTD
tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN,
kumpongeza kwa kuadhimisha miaka MITATUmadarakani.
INTRODUCING
LONG LASTING CERAMIC DIGITAL
PRINTING ON GLASS
ALSO LOCALLY MANUFACTURED
SALEHBHAI
TUFF GLASS
SALEHBHAI
LAMI GLASS
KOOLPANE
DOUBLE
GLAZE UNIT
SALEHBHAI
DESIGNER
locally
MADE
CONTACT US
Aggrey/Indira Gandhi street / P.O.Box 40917 / Dar es salaam / +255 763 501 771 /+255 22 211 5859
+255763501771
Salehbhai_glass_industries_ltd
salehbhaiglass@hotmail.com
www.salehbhaiglass.co.tz

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars sasa izingatie wengi wa ndani kwa ajili ya CHAN

**KIKOSI** cha wachezaji 23 kilichoitwa wiki iliyopita na Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Morocco, kwa mechi zilizopo kwenye Kalenda ya FIFA, kimeondoka Dar es Salaam leo kuelekea nchini Azerbaijan kwa ajili ya mechi za kirafiki.

Ukikiangalia kikosi hicho kimejaa wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi licha ya kutoorodheshwa kwa nahodha, Mbwana Samatta.

Sisi tulidhani kwa sababu nchi inajiandaa kuwa mwenyeji wa fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Septemba mwaka huu, tulitegemea kuwe na wachezaji wengi wanaocheza soka nchini na si wa nje.

Hatukatai wachezaji wa nje, lakini kwa sababu tunaelekea kujiandaa na CHAN mwezi Septemba na inafanyika hapa hapa nchini, maandalizi yalitakiwa yafanyike sasa kwa wale wa ndani wengi ili kuendelea kupata uzoefu.

Wakati serikali ikijiandaa na maandalizi ya miundombinu, ikiwamo viwanja, maandalizi mengine yanatakiwa yawe ndani ya uwanja, kwa kukiandaa kikosi kabambe cha wachezaji ambao tayari wameshaiva kucheza michuano hiyo.

Haiwezekani tuingie kwenye michuano ya CHAN tukiwa na wachezaji ambao hawajacheza japo mechi tano za kirafiki za kimataifa zilizo katika Kalenda ya FIFA, halafu tutegemee kufanya vizuri.

Nadhani hatuandai CHAN ili timu zije kulichukua kombe, bali hata sisi wenyewe tunalihitaji, hivyo tunahitaji mikakati kabambe, ikiwamo kuisuka timu yenye wachezaji bora na waliojiandaa kikamilifu.

Hata kama watulichukua, lakini Tanzania ionyeshe kuwa ilikuwa na dhamira ya dhati ila tu wenzetu wametuzidi mbinu na ubora, lakini isiwe ni kwa sababu ya kutokuwa na wachezaji wenye uzoefu na mechi za kimataifa.

Hata hivyo, tayari makosa hayo yamefanyika, rai yetu sasa ni kuona Kalenda za FIFA zijazo, makocha wa Stars, wakiliangalie hilo kwa umakini ili kujenga kikosi imara kitakachokwenda kuleta mafanikio chanya CHAN kama ambavyo wenzetu Ivory Coast walivyoonyesha ni namna gani mwenyeji anapaswa kufanya baada ya kuutwaa ubingwa wa Mataifa ya Afrika (Afcon), mwaka huu wakiwa wenyeji wa michuano hiyo.

Tunaamini umefika wakati wa kupunguza wachezaji wa wanaocheza nje ya nchi kwa muda, na kuchagua wa ndani kwa ajili ya malengo ya CHAN ili tusiwe wapenzi watazamaji, au wasindikizaji, badala ya kuwa washindani.

Ukiondoa wachezaji wa Simba, Yanga na Azam ambao wana uzoefu wa mechi za kimataifa, wachezaji wa timu nyingi zilizobaki hawana, hivyo ulikuwa ni wakati muafaka kwao kuanza kutumika katika kalenda hii.

Mfano kuna straika ambaye kwa sasa anafanya vizuri kwenye Ligi Kuu, Samson Mbangula wa Prisons, huyu alitakiwa awamo kwenye kikosi cha Taifa Star skwa sasa ili apate ladha halisi ya michuano hiyo ili hata kama akiitwa baadaye kwa ajili ya CHAN asiwe mgeni wa mechi za kimataifa.


Wapo wachezaji ambao tunadhani wanaweza kuitwa baadaye kwa ajili ya CHAN kama kina Kelvin Kijili na wengineo wengi ambao wapo vikosi ambavyo huwa havichezi mechi za kimataifa kama ilivyo wale wanaotaka Simba na Yanga, hao wanatakiwa waitwe wakiwa ili kupata mikikimikiki ya michuano ya kimataifa kwa ajili ya kuiwakilisha vema nchi.

Ni wazi kwa hili makocha wa Stars wameteleza, hivyo kalenda ijayo tunaamini wataona umuhimu huo na kuanza maandalizi ya kikosi cha CHAN.

Ikumbukwe tutakapocheza CHAN hatutakuwa na mchezaji yeyote anayecheza soka la kulipwa nje, kwa hiyo ni wakati wa kuwateua wa ndani mapema ili nao wapate uzoefu wa kucheza mechi kadhaa kabla ya CHAN ya mwaka huu ambayo Tanzania ni mwenyeji, ikishirikiana na Kenya na Uganda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ayoub anavyowasuta mashabiki, Guede, Freddy wapewe muda

**KWA** sasa ukiwauliza mashabiki wa Simba katika mechi ngumu kipa gani wanataka akae langoni, watakujibu, Ayoub Lakred, jibu hili usingeweza kulisikia katika mechi za mwanzo za msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ayoub, raia wa Morocco ambaye pia ni mmoja wa wachezaji wachache kama si pekee kucheza Ligi ya Tanzania kutokea Afrika Kaskazini, maarufu kama 'nchi za Kiarabu' alibezwa sana na kupewa kila aina ya kejeli mwanzoni wakati amejiunga na Simba, hata aliposimama langoni mechi za mwanzo.

Mashabiki wa Tanzania na hata baadhi ya wachambuzi walimfanyia kila aina ya dhihaka, wakisema hana hadhi ya kudakia timu kubwa kama Simba.

Binafsi, ilinipa shaka kidogo kwa sababu timu alizozichezea kabla ya kutua Simba ni kubwa kama anayoichezea miamba hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Dar es Salaam.

Ameidakia RS Berkane ya Morocco, akijiunga nayo 2014, kabla ya 2019 kujiunga na FAR Rabat ya nchini humo.

Ilinipa mshangao na kujiuliza, kipa aliyezidakia klabu hizo mbili ambazo ni maarufu sana kwenye soka, akaaminiwa kukaa kwenye milingoti mitatu, leo ashindwe kukaa kwenye lango la Simba?

Hakufanya vema mwanzoni kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na hata Ligi Kuu, lakini taratibu baadaye alianza kubadilika. Leo hii wala sitafuni maneno au kuzunguka nikisema ndiye kipa namba moja wa Simba.

Waswahili wana msemo wao kuwa dunia inakwenda kasi sana, leo hii wanachama na mashabiki wa Simba wanapoona jina la Ayoub kuwa anakaa langoni wanafurahi na kushusha presha.

Ametokea kuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Simba ambao wamekuwa na imani naye, yeye pia sasa hawaangushi.

Mpaka sasa kwenye Ligi Kuu ana 'clean sheet' tano, akiwa mmoja wa makipa aliyesimama langoni mechi nyingi bila kuruhusu bao akiwafukuza wengine juu.

Haikuwa rahisi kwake kufika hapo, badala yake amepitia kwenye mazingira magumu na ya kukatisha tamaa.

Nadhani mwanzoni alikuwa na tatizo la mawasiliano na wenzake, kutozeana nao, yeye mwenyewe kutofahamu mazingira mbalimbali yanayomkabili hasa ikizingatiwa ni mara ya kwanza kucheza soka katika nchi ambazo si za Kiarabu, pia hali ya hewa, viwanja, vyakula, miundombinu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Nafikiri kwa sasa ameshafahamu kila kitu, amezoea mazingira, wenzake na vitu vingi kiasi kwamba kiwango chake kile kilichomfanya aaminiwe na FAR Rabat na RS Berkane kuonekane.

Mechi ya ugenini dhidi ya Wydad Casablanca, Ligi ya Mabingwa Afrika, dhidi ya Azam, JKT Tanzania, Mashujaa FC na Singida Fountain Gate, ni moja kati ya michezo bora kabisa kwake iliyomfanya kuheshimika nchini.

Hili nalirudisha kwa baadhi ya wachezaji waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo na Klabu za Simba na Yanga.

Mashabiki wa Simba wanaonekana kulia na Freddy Michael kuwa hana uwezo ambao waliutarajia, wanaenda mbali na kusema ni bora Jean Baleke au Moses Phiri mmoja wao asingeachwa.

Kwa upande wa Yanga, Joseph Guede, amekuwa akipingwa kuwa si aina ya straika waliyekuwa wakimhitaji kumlinganisha na Fiston Mayele aliyeondoka.

Cha ajabu ni kwamba Guede ndiye aliyefunga bao lililoipeleka Yanga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Freddy akiwa na mabao matatu kwenye Ligi Kuu.

Mashabiki wanarudi kule kule kwa Ayoub. Wakati mwingine tusiwajaji wachezaji wanapocheza mechi moja, mbili au tatu, badala yake wanahitaji muda wa kutosha ili kuonyesha walichonacho.

Ni kweli kuna wachezaji wanapofika tu kwenye timu wanaanza kwa moto, lakini wengine wanahitaji muda. Hata Mayele alihitaji muda, Heritier Makambo, akionekana bora zaidi kuliko yeye. Siku zote muda ndiyo hakimu wa haki. Tusubiri muda utaongea.

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

Head Office: PSSSF Millennium Towers II, Bagamoyo Road
P.O Box. 9300, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: +255 22 2162940 Fax: +255 22 2114815
website: www.tcbbank.co.tz
Emal: ceo@tcbbank.co.tz

# JOB VACANCIES

**ABOUT US:**

Tanzania Commercial Bank is a Bank that provides competitive financial services to our customers and creates value for our stakeholders through innovative products with a vision "to be the leading bank in Tanzania in the provision of affordable, accessible and convenient financial services". As part of organizational development and management of its human capital in an effective way, Tanzania Commercial Bank commits itself towards attaining, retaining and developing the highly capable and qualified workforce for Tanzania Commercial Bank betterment and the Nation at large.

| | |
|---|---|
| Position: | Director of Retail and SME Banking |
| Department: | Retail and SME Banking |
| Reports to: | Chief Executive Officer |
| Level: | Director |
| Location: | Head Office Dar- Es -Salaam |

**POSITION FUNCTION:**

Provide a wide variety of excellent retail and SME banking services to our existing and potential customers. Emphasize customer-oriented offers and modern distribution channels to stand out and provide top-notch Retail and SME banking services.

**KEY RESPONSIBILITIES**

(i) Create, implement, and oversee retail and SME strategy and business plan, considering market potential, competition, capabilities, and risk tolerance.
(ii) Determine target markets and customer offers, as well as product and sales mix. Establish measurable business growth goals, management processes, and performance metrics.
(iii) Foster a service-oriented sales culture and analyse Tanzania's potential, including physical and self-service channels.
(iv) Expand business through service outlets, agents, and partners.
(v) Ensure compliance with bank policies, review and develop policies, operational systems, and internal controls.
(vi) Enhance customer service through process reengineering and satisfaction surveys.
(vii) Develop work plans for banking department divisions, monitor implementation and evaluation.
(viii) Maintain and optimize support systems and infrastructures.
(ix) Identify and mitigate operational and other risks within the department.
(x) Identify and address staff training needs to improve productivity.
(xi) Implement customer retention and loyalty programs.
(xii) Build and guide motivated teams through counselling, mentoring, and guidance.

**QUALIFICATIONS, SKILLS AND EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Business Administration, Finance, Accounting, Banking, Economics, Commerce and Marketing or equivalent qualifications from recognized institutions. (Master's degree is an added advantage

> A minimum of ten (10) years working experience in Banking Industry or Financial Institutions and at least two years in Managerial Position.
> Strong strategic thinking and analytical skills, with the ability to translate insights into actionable plans.
> Excellent communication and interpersonal skills, with the ability to inspire and motivate teams.
> Deep understanding of banking regulations, compliance requirements, and risk management principles.
> Experience in driving digital transformation initiatives and leveraging technology to drive business results.

| | |
|---|---|
| Position: | Manager Digital & Innovation |
| Department: | Digital & Innovation |
| Reports to: | Chief Executive Officer |
| Level: | Manager |
| Location: | Head Office Dar- Es -Salaam |

**POSITION OBJECTIVE**

To drive digital transformation and foster innovation within the organization by leveraging emerging technologies, enhancing operational efficiency, and delivering cutting-edge solutions that empower teams, delight customers, and propel sustainable growth in a rapidly evolving digital landscape.

**KEY RESPONSIBILITIES**

(i) Lead teams in innovation and Implementation of Operational Efficiency Strategies through automation of manual processes to ensure smooth operation of products
(ii) Inspire and drive other departments automation of processes through sharing of technical expertise on digital solutions implementations;
(iii) Active engagements with colleagues for business proposals writing to access donor and stakeholders funding on digital products;
(iv) Provide lead and roadmap to the financial inclusion projects – partners and donor funds projects management of financial inclusion;
(v) Create and enhance system solutions to meet bank's goals and strategies
(vi) Responsible for the improvement of processes and automation so as to create efficiency, Turnaround time (TAT), customer services and compliance aspect;
(vii) Responsible for the implementation of the critical projects for the bank within the agreed time frame and allocated budgets;
(viii) Oversee implementation of changes in digital environment in a way that minimizes disruptions to the bank's services;
(x) Ensure appropriate policies, procedures and processes are followed when it comes to software development;
(xi) Monitor, evaluate and ensure the completion of tasks and projects; analyses software requirements; implements design plans, reviews unit tests;
(xii) Document's software development;
(xiii) Monitor status of developing software;
(xiv) Writes, Reviews and Revises product requirements and specifications;
(xv) Participates in other areas of the software development process; and provides technical support to other company personnel if necessary;
(xvi) Prepare Documentation/ Technical authoring such as business requirement specifications, project certification, project closure reports, investigation reports; and
(xvii) Ensure software is updated with the latest features.

**QUALIFICATIONS, SKILLS & EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Business Information Technology, Innovation Management, Arts in Design, Arts in Economics, Arts in Digital Media, Arts in Graphics Design, Computer science, Electronic Science & Communication, Computer Engineering Information & Technology, Electronics Engineering, Telecommunication Engineering, Commerce or equivalent qualifications from recognized institutions. Must at least eight (8) years working experience in Banking Industry or Financial Institutions. (Master's degree is an added advantage).

> Strong understanding of project management methodologies and best practices, with experience.
> Excellent leadership and interpersonal skills, with the ability to effectively collaborate with diverse stakeholders and motivate cross-functional teams.
> Exceptional organizational and problem-solving abilities, with a keen attention to detail and a focus on delivering high-quality results.
> Proficiency in project management tools and software, such as Microsoft Project and familiarity with relevant technology platforms and systems.

| | |
|---|---|
| Position: | Project Manager |
| Department: | Project Management |
| Reports to: | Chief Executive Officer |
| Level: | Manager |
| Location: | Head Office Dar- Es -Salaam |

**POSITION OBJECTIVE**

Provide a wide variety management of projects from inception to completion, utilizing skills in planning, coordination, and team leadership to deliver high-quality results on time and within budget. With a focus on clear communication, risk mitigation, and stakeholder engagement, also to drive project success and exceed expectations while fostering a collaborative and motivating work environment.

**KEY RESPONSIBILITIES**

(i) Developing detailed project plans to guide staff members and project teams and revising based on changing needs and requirements;
(ii) Plan, execute and supervise projects to meet Bank goals and success markers
(iii) Identify and assigning project tasks based on skill sets, experience and strengths of staff members;
(iv) Manage the project team;
(v) Monitor project milestones, timeline and budget are met and adhered to;
(vi) Developing excellent leadership, customer relations and communication skills to liaise effectively with all projects stakeholder.
(vii) Provide lead and roadmap to the digital products implementation and financial inclusion projects – partners and donor funds projects management of financial inclusion;
(viii) Work effectively with relevant stakeholders for efficient project implementation;
(ix) Communicate effectively with stakeholders and providing reports on project progress;
(x) Compile and submit projects status reports to clients, management and other stakeholders;
(xi) Manage project documentation and ensuring resource availability and allocation;

**QUALIFICATIONS, SKILLS & EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Project Management, Business Information Technology, Computer science, Electronic Science & Communication, Computer Engineering Information & Technology, Electronics Engineering, Telecommunication Engineering, & statistics or equivalent qualifications from recognized institutions. Must at least eight (8) years working experience in Banking Industry or Financial Institutions. (Master's degree is an added advantage).

> Strong understanding of project management methodologies and best practices, with experience.
> Excellent leadership and interpersonal skills, with the ability to effectively collaborate with diverse stakeholders and motivate cross-functional teams.
> Exceptional organizational and problem-solving abilities, with a keen attention to detail and a focus on delivering high-quality results.
> Proficiency in project management tools and software, such as Microsoft Project and familiarity with relevant technology platforms and systems.

**PERSONAL ATTRIBUTES AND BEHAVIOURAL COMPETENCIES**

> Ability to demonstrate Tanzania Commercial Bank core values:
> Customer Focus, trustworthy, Creativity, Teamwork and Excellence
> Ability to priorities work and to meet deadlines.
> Ability to work quickly, accurately and consistently when under pressure.
> A methodical and well-organized approach to work.
> Mature and able to work in a confidential environment.
> Has sound judgment, common sense and good humour.

These positions will attract a competitive salary and fringe benefits.

Applicants are invited to submit their resume via the following link:- **https://www.tcbbank.co.tz/careers** Applications via other methods will not be considered. Applicants need to fill their personal information, academic certificates, work experiences, and application letter. Other credentials will be submitted during the interview for authentic check & administrative Measures.

Tanzania Commercial Bank has a strong commitment to environmental, health and safety management. Late applications will not be considered. Short listed candidates may be subjected to any of the following: a security clearance; a competency assessment and physical capability assessment.

**Deadline of the Application is 1st April, 2024.**

# Makaburi ya watu 88 waliofariki ajali ya treni yageuzwa maficho ya vibaka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IKIWA ni takriban miaka zaidi ya 20 tangu kutokea ajali ya treni eneo la kati ya Stesheni ya Msagali na Igandu mkoani Dodoma, wakazi wa Mtaa wa Mathias, Kata ya Miyuji wamelalamikia Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuyatelekeza makaburi ya waathirika wa ajali hiyo, hata kutumika kama maficho ya vibaka.

Ajali hiyo ilitokea Juni 24, 2002 ambapo katika eneo hilo kuna makaburi ya watu 88 kati ya 288 wa ajali hiyo.

Nipashe ilitembelea eneo hilo mwishoni mwa wiki na kubaini makaburi hayo hayajafanyiwa usafi kwa muda mrefu na hivyo kuzingirwa na vichaka vikubwa vinavyotumika kama maficho ya uhalifu na kutishia hali ya usalama.

Mmoja wa wananchi hao, Hilary Mark alisema kuna vichaka vikubwa ambavyo vinatumika kama maficho ya vibaka na wavuta bangi.

"Wakati huu ambao mvua inanyesha, vichaka ni vikubwa, limekuwa ni eneo la watu kujificha kwa kuwa unapopita ni eneo tulivu, halina msongamano wa watu, kiusalama hali si nzuri maana halina ulinzi, alisema.

Ismail Israel, mwenye makazi jirani na eneo hilo, alisema serikali za mitaa na TRC ambao wana wajibu wa kusimamia eneo hilo wamejisahau eneo hilo.

Mkazi wa Ipagala, Gersha Muhango aliomba watu wenye mamlaka kuliangalia eneo hilo na si kutekeleza makaburi hayo.

"Eneo hili wenzetu wamehifadhiwa sisi tulio hai, wajibu wetu ni kulifanyia usafi na si kuliacha na kuhatarisha usalama wa wananchi," alisema.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Sikuzani Daudi, alisema vitu mbalimbali vilivyokuwapo ikiwamo kichwa cha treni kilichotengenezwa kwa chuma, viliibwa.



Wafanyabiashara wadogo katika kituo cha mabasi, Nzega mjini wakiwashawishi abiria waliokuwa ndani ya basi kununua bidhaa zao juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kamati ya Bunge yataka magari yanayoletwa nchini yawe ya gesi

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeshauri serikali na wauzaji binafsi wa magari kujipanga kuagiza vyombo vya moto vinavyotumia mfumo wa gesi.

Pia imeshauri serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuunganisha au kubadili mfumo wa magari kutoka mafuta kwenda gesi asilia, ili kuvutia Watanzania wengi kubadili mfumo wa magari yao.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. David Mathayo wakati kamati hiyo ilipotembelea vituo vya kujaza gesi asilia.

Dk. Mathayo alisema serikali inapaswa kuongeza vituo vya kujazia gesi asilia kwenye magari kwa kuwa hivi sasa ni vichache na havikidhi mahitaji. Idadi ya magari yanayotumia gesi imekuwa kubwa.

"Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tungependa kulishauri Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC) na serikali kwa ujumla waendelee kuhamasisha vituo vya kujaza gesi asilia viwe vya kutosha kwa sababu kadri miezi inavyozidi kusogea, wahitaji nao wanaongezeka," alisema Dk. Mathayo.

Vilevile, alisema serikali inapaswa kuondoa kodi kwa vifaa vinavyotumika katika kuunganisha au kubadili mifumo ya mafuta kwenda gesi asilia ili Watanzania wengi wabadilishe magari yao yatumie gesi.

"Hivi sasa kubadili mfumo ni Sh. milioni 1.8 hadi Sh. milioni mbili. Kwahiyo, vifaa vile vikipunguzwa bei ni dhahiri kwamba wananchi wengi watahamasika kubadilisha mifumo ya magari yao na kutumia gesi," alisema Dk. Mathayo.

Kamati hiyo ilishauri serikali kuhamasisha wale wanaouza magari kuleta yaliyobadilishwa mifumo katika viwanda yanakotengenezwa.

Pia alipongeza serikali kwa kuanzisha matumizi ya gesi asilia katika magari yake, akisema gesi asilia gharama yake iko chini kulinganishwa na mafuta ya kawaida kama petroli na dizeli; gari linalotumia gesi asilia linakwenda umbali mrefu likitumia fedha kidogo.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alishukuru kamati hiyo na kusema serikali imepokea ushauri na mapendekezo yaliyotolewa.

Alisema serikali kupitia TPDC ina mkakati wa kuendelea kuongeza vituo vya kujazia gesi asilia, akisema hadi sasa kuna vituo vitano. Alisema kuna vituo 15 vilivyo katika mchakato na vinaendelea kujengwa ili wananchi wanufaike zaidi na kupunguza msongamano.

Judith alisema serikali ina mkakati wa kushirikiana na washirika binafsi, kampuni kuendelea kuongeza karakana za kubadilisha mifumo ya magari. Mkurungenzi Mtendaji wa TPDC, Mussa Makame, alisema wako katika mchakato wa kununua vituo vitano vinavyotembea vya kujaza gesi hiyo katika magari. Vitasambazwa katika maeneo mbalimbali.

Makame alisema vituo 15 vya kujaza gesi asilia vinatarajiwa kujengwa mkoani Dar es Salaam, lengo likiwa ni kuondoa changamoto ya msongamano katika vituo vilivyopo.

## UVCCM wajitosa ufuatiliaji matumizi fedha za miradi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Mohamed Kawaida, amesema jumuiya hiyo imeanza utekelezaji wa kufuatilia fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi kwenye halmashauri zote nchini.

Kawaida aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua mdahalo wa siku mbili wa Seneti ya Vyuo na Vyuo Vikuu uliofanyika Ukumbi wa Chuo cha Ufundi Ihemi kinachomilikiwa na UVCCM kilichoko wilayani Iringa.

Mdahalo huo ulihusisha vyuo na vyuo vikuu nchi nzima ikiwa ni maandalizi ya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa viongozi wa seneti hiyo uliofanyika juzi.

Kawaida alitaka vijana wachangamkie fursa zinazotolewa na serikali, akieleza kuwa jumuiya hiyo itahakikisha fedha zilizotolewa na serikali zinafika kwa walengwa na kufanya kazi iliyokusudiwa, zikiwamo zinazohusu miradi ya vijana.

Kawaida alisema: "Hivi karibuni Mheshimiwa Rais amefanya mambo mawili; ameanzisha mradi wa BBT ambao unaendelea vizuri katika utekelezaji wake licha ya changamoto ndogo zilizojitokeza katika kutekeleza mradi huo, na kutoa fedha kwa kila halmashauri zetu nchini".

Kutokana na kutolewa fedha hizo, Kawaida alitaka vijana kuchangamkia fursa ya kuomba tenda ili wanufaike na fedha hizo zinatolewa nchini kote.

Kawaida aliwasihi vijana nchini kuacha kutumika kwa mwamvuli wa ahadi za ajira kwa kuwa tatizo la ajira ni la dunia nzima na si Tanzania pekeKawaida alikemea vitendo vya wanasiasa kutumia vijana ili kusukuma ajenda zao na kujinufaisha.

"Vijana amkeni, msikubali kutumika kusukuma ajenda za watu ili waweze kufanikisha mambo yao kwa maslahi yao binafsi. Serikali yenu ya awamu ya sita inaendelea kuchukua jitihada mbalimbali kuhakikisha vijana mnapata mikopo ili mjikwamue kiuchumi," alisema Kawaida.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, akiwasilisha mada kwenye mdahalo huo inayohusu Mchango wa Wasomi katika Siasa na Maendeleo ya Taifa', alisema vijana wasomi wanalo jukumu la kuwa na uhuru wa kutoa maoni ili wanapokosea na kukoselewa wajifunze.

Alisema kukosea ndio mwanzo wa kujifunza, hivyo vijana wakikosea isiwe chanzo cha kuwatengenezea usaliti.

"Inashangaza kuona vijana wakikosea, matokeo yao wanaambiwa "mpinzani". Kwa kufanya hivyo kunapelekea vijana kuingiwa na uoga wa kuongea na kutoa maoni yao," alihadharisha.

TANGAZO

TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC TACOBA "Our Bank for Our Development"

# BENKI YA WANANCHI TANDAHIMBA

# TAARIFA ZA HESABU ZILIZOKAGULIWA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha '(Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE - 31 DESEMBA, 2023

(Kiasi kwa Shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/12/2023 | Robo mwaka iliyopita 30/09/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 263,191 | 8,101 |
| 2. | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,566,968 | 752,683 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 2,854,476 | 3,030,268 |
| | (Net of Allowances for Probable Losses) | 0.00 | 0 |
| 12 | Mali Nyingine | 352,194 | 178,712 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 155,440 | 156,990 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **5,192,269** | **4,126,754** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,711,275 | 871,986 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo /Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 131,665 | 63,010 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baa | 91,143 | 104,180 |
| 27 | Dhima Nyingine | 50,542 | 30,342 |
| 28 | Madeni | 871,147 | 797,813 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **2,855,772** | **1,867,331** |
| 30 | **MALI/ DHIMA HALISI (16 kutoa 29)** | **2,336,497** | **2,259,423** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 4,483,228 | 4,483,228 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yalibakizwa | (2,327,779) | (2,348,098) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 65,901 | -11,172 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 115,147 | 135,465 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,336,497** | **2,259,423** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 80,748 | 56,259 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 51,555 | 35,116 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 45.0% | 54.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.77% | 1.83% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi Halisi na Jumla ya Amana | 169.8% | 351.5% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.0% | 73.4% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.2% | 91.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 96.3% | -18.1% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 25.8% | 7.5% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 31 DESEMBA, 2023

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/12/2023 | Robo mwaka Iliyopita 31/12/2022 | Mwaka wa Sasa 31/12/2023 | Mwaka Uliopita 31/12/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Riba | 170,775 | 109,232 | 555,251 | 522,070 |
| 2. | Gharama za Riba | (30,381) | (22,605) | (84,717) | (47,878) |
| 3. | **Mapato Halisi ya Riba ( 1 kutoa 2)** | **140,394** | **86,627** | **470,534** | **474,192** |
| 4. | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (12,390) | (95,964) | 31,959 | (83,147) |
| 6. | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **166,116** | **107,175** | **259,088** | **253,128** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 166,116 | 107,175 | 259,088 | 253,128 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7. | **Gharama Zisizo za Riba** | **(188,803)** | **(183,812)** | **(667,436)** | **(661,178)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (52,022) | (60,228) | (212,928) | (242,996) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (136,781) | (123,584) | (454,508) | (418,183) |
| 8. | **Faida / (Hasara) Halisi ya Uendeshaji** | **105,317** | **(85,974)** | **94,145** | **-17,005** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (28,243) | 20,691 | (28,243) | (3,807) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **77,074** | **(65,283)** | **65,901** | **(20,813)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 77,074 | (65,283) | 65,901 | (20,813) |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 16 | 15 | 16 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 17 | (15) | 15 | -5 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i)Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 8.1% | -9.9% | 1.8% | -0.5% |
| | (ii)Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 13.3% | -11.3% | 2.9% | -0.9% |
| | (iii)Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 61.6% | 94.8% | 35.5% | 90.9% |
| | (iv)Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 15.8% | 11.7% | 12.8% | 16.3% |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA - 31 DESEMBA, 2023

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa-31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,339,556) | 173 | - | 153,306 | 2,297,150 |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 65,901 | - | - | - | 65,901 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (639) | 639 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 12,417 | - | - | (38,972) | (26,555) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,261,877) | 812 | - | 114,335 | 2,336,497 |
| **Mwaka uliopita-31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,392,795) | 74,225 | - | 87,456 | 2,252,113 |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (20,813) | - | - | - | (20,813) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 74,052 | (74,052) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | 65,850 | 65,850 |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,339,556) | 173 | - | 153,306 | 2,297,150 |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 31 DESEMBA, 2023

(Kiasi kwa Shilingi Maelfu)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 31/12/2023 | Robo Mwaka Iliyopita 30/09/2023 | Mwaka wa Sasa 31/12/2023 | Mwaka Uliopita 31/12/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 105,317 | 47,146 | 94,145 | (17,005) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara katika Mali | 24,136 | (15,845) | 40,795 | 150,544 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 222,842 | (293,061) | (473,430) | 271,848 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi katika Amana | 835,811 | (189,383) | 533,652 | (79,175) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | - | - | - |
| | za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 79,629 | 147,522 | 273,692 | (118,869) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (173,482) | (50,755) | (215,468) | 161,084 |
| | - Kodi iliyolipwa | (31,750) | - | (25,750) | 40,680 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 8,505 | (26,129) | (54,359) | (288,802) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,071,008** | **(380,505)** | **173,277** | **120,304** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | Gawio Lilopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (3,821) | - | (32,359) | (636) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | (8,231) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji** | **(3,821)** | **-** | **(32,359)** | **(8,867)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lilolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 2,188 | 297,813 | 800,000 | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **2,188** | **297,813** | **800,000** | **-** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,069,375 | (82,692) | 940,917 | 111,437 |
| | Fedha Taslimu na Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 760,784 | 843,476 | 889,242 | 777,805 |
| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **1,830,159** | **760,784** | **1,830,159** | **889,242** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2023

Hapo juu ni taarifa za Fedha za Benki zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba,2023 ambazo zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya makampuni, Namba 12 ya mwaka 2002 CAP 212.
Taarifa hizi za Fedha zimekaguliwa na wakaguzi wa nje Auditax International - Certified Public Accountants (T) na kupata hati safi.

| | Tarehe | Saini |
|---|---|---|
| Yahya J. Kiyabo<br>**Meneja Mkuu** | 12/03/2024 | |
| Julius J. Sawaya<br>**Mkuu wa Fedha na Uendeshaji** | 12/03/2024 | |
| Aloyce Leonard<br>**Mkaguzi wa Ndani** | 12/03/2024 | |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Tarehe | Saini |
|---|---|---|
| Mohamed N. Mwinguku<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | 12/03/2024 | |
| Mariam S. Mwanzalima<br>**Mjumbe wa Bodi** | 12/03/2024 | |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| Sn | BANK CHARGES 2023 Transactions | Description | Previous Rates 2023 VAT Exclusive | Previous Rates 2023 VAT Inclusive | New Rates 2023 VAT Exclusive | New Rates 2023 VAT Inclusive |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Account Maintenance Fee** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 2,500 | 2,950 | 2,500 | 2,950 |
| | Company Savings | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | **Group saving** | | | | - | - |
| | Amcos Collection | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | Amcos Business | Per Month | Free | Free | Free | Free |
| | Local council | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | Group saving | Per Month | 3,500 | 4,130 | 3,500 | 4,130 |
| 2 | **Min account Opening** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a | 20,000 | N/a |
| 3 | **Min operating Balance** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a | 20,000 | N/a |
| 4 | **Cash withdral Over the counter** | | | | | |
| | From TZS 1,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-9,999 | Per transaction | 750 | 885 | 750 | 885 |
| | From TZS 10,000-19,999 | Per transaction | 1,200 | 1,416 | 1,200 | 1,416 |
| | From TZS 20,000-39,999 | Per transaction | 1,650 | 1,947 | 1,650 | 1,947 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,500 | 4,130 | 3,500 | 4,130 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 4,500 | 5,310 | 4,500 | 5,310 |
| | From TZS 200,000-299,999 | Per transaction | 5,500 | 6,490 | 5,500 | 6,490 |
| | From TZS 300,000-599,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 600,000-799,999 | Per transaction | 7,000 | 8,260 | 7,000 | 8,260 |
| | From TZS 800,000-999,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 1,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 3,000,000-4,999,999 | | 9,500 | 11,210 | 9,500 | 11,210 |
| | 5,000,000 - Above | | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 |
| | Mwana A/C cash withdrawal exceeding 3rd transaction per annum | Per transaction | 3,000 | 3,540 | 3,000 | 3,540 |
| 5 | **Cash withdral - TACOBA Agency Banking** | | | | | |
| | From TZS 0-499 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 500-999 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 1,000-1,999 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 2,000-2,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 3,000-3,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 4,000-4,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-6,999 | Per transaction | N/a | N/a | 700 | 826 |
| | From TZS 7,000-9,999 | Per transaction | N/a | N/a | 700 | 826 |
| | From TZS 10,000-14,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 15,000-19,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 20,000-29,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 30,000-39,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | N/a | N/a | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | N/a | N/a | 3,200 | 3,776 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | N/a | N/a | 3,950 | 4,661 |
| | From TZS 200,000-239,999 | Per transaction | N/a | N/a | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 240,000-299,999 | Per transaction | N/a | N/a | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 300,000-399,999 | Per transaction | N/a | N/a | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 400,000-499,999 | Per transaction | N/a | N/a | 6,800 | 8,024 |
| | From TZS 500,000-599,999 | Per transaction | N/a | N/a | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 600,000-699,999 | Per transaction | N/a | N/a | 7,700 | 9,086 |
| | From TZS 700,000-799,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 800,000-899,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 900,000-999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,500 | 10,030 |
| | From TZS 1,000,000-1,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 2,000,000-2,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 3,000,000-3,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 4,000,000-4,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 5,000,000-5,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 10,000 | 11,800 |
| | From TZS 6,000,000-6,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 11,000 | 12,980 |
| | From TZS 7,000,000-7,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 12,500 | 14,750 |
| | From TZS 8,000,000-8,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 14,000 | 16,520 |
| | From TZS 9,000,000-9,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 15,000 | 17,700 |
| | From TZS 10,000,000 & Above | Per transaction | N/a | N/a | 15,000 | 17,700 |
| 6 | **Activation of Dormant Accounts** | | | | | |
| | All other accounts | Free | Free | Free | Free | Free |
| | Saving account of personal loan customers | Per account | Free | Free | Free | Free |
| 7 | **Closing of Account** | | | | | |
| | Saving account | Per account | 5,000 | 5,900 | 5000 | 5900 |
| | All other accounts | Per account | 10,000 | 11,800 | 10000 | 11800 |
| 8 | **Inter-Bank (Outward Funds Transfer)** | | | | | |
| | TISS | Per transaction | 10,000 | 11,800 | 10000 | 11800 |
| | **Inter-Bank (Inward Funds Transfer)** | | | | | |
| | Internal Transfer | Per transaction | 1,000 | 1,180 | 1000 | 1180 |
| 9 | **Cards** | | | | | |
| | **New Cards** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 | 11,000 | 12,980 |
| | **New Cards due to expired** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 | 11,000 | 12,980 |
| | **Peplacement due to lost/spoiled** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 10,000 | 11,800 | 10,000 | 11,800 |
| | Korosho card | Per card | 22,000 | 25,960 | 22,000 | 25,960 |
| | Annual card fee All Cards | per card | 10,000 | 11,800 | 10,000 | 11,800 |
| 10 | **Account statements** | | | | | |
| | Interim statement per month | per transaction | Free | Free | Free | Free |
| | Quartely statement | per transaction | 2,500 | 2,950 | 3,000 | 3,540.00 |
| | Adhoc from 4 up to 12 month | per transaction | 10,000 | 11,800 | 15,000 | 17,700.00 |
| | Adhoc above 12 month | per transaction | 20,000 | 23,600 | 20,000 | 23,600 |
| 11 | **Salary and Bulk payment** | | | | | |
| | Salary and Bulk payment fee | per transaction | 4,500 | 5,310 | 3,000 | 540 |
| | Transfer to other Banks | per transaction | 5,000 | 5,900 | 5,000 | 900 |
| | Balance enquiry | per request | 500 | 590 | Free | Free |
| 12 | **Information search** | | | | | |
| | For information up to 12 past months | per document | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | For information of 1 to 5 past years | per document | 80,000 | 94,400 | 80,000 | 94,400 |
| | For information above 5 years | per document | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| | CCTV Image retrieve | Per request | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| 13 | **Introduction Letter and certificate of Balance** | | | | | |
| | Cerfificate of balance | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | status report | per report | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Visa recommendation | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Any other introduction | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Bank statement requested by other banks | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| 14 | **Loan Fees** | | | | | |
| 1 | **MSE** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% | | 1% | |
| | Facility Fee | | 1% | | 1% | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% | | 1% | |
| 2 | **AGRICULTURE LOANS** | | | | | |
| | Loan fee | 0-999,999 | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| | Loan fee | 1mn - 1,999,999 | 200,000 | 236,000 | 200,000 | 236,000 |
| | Loan Application fee | 2mn and above | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| 3 | **PERSONAL LOAN** | | | - | | |
| | Loan Application fee | | 0.55% MIN 55,000 | | 0.55% MIN 55,000 | |
| | Facility Fee | | 1% MIN 90,000 | | 1% MIN 90,000 | |
| | Legal documentation fee | | Free | | Free | |
| 4 | **GROUP LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| 5 | **ASSET FINANCING LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% on Loan amount | | 0.5% on Loan amount | |
| 6 | **CHAPCHAP LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | Free | | Free | |
| | Facility Fee | | | 3% Min 59,000 VAT INCL | 0% | |
| | Legal documentation fee | | Free | | Free | |
| 15 | **charges on early loan payment** | | | | | |
| | Salary loan | | 5.9% min 500,000 | | 5.9% min 500,000 | |
| | MSE business loan | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | |
| | Agriculture loan | | Free | | Free | |
| | Other segment | | 3% on the unpaid amount | | 3% on the unpaid amount | |
| | Restructuring Fee | | 2% min 150,000 | 177,000 | 2% min 150,000 | 177,000 |
| 16 | **Cheque Book order** | | | | | |
| | Per leaf - 100 | | 1,000 | 1,180 | 1,000 | 1,180 |



# Ucheleweshaji mashauri wamchefua Naibu Katibu Mkuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Khatibu Kazungu, amechukizwa na hali ya ucheleweshwaji wa mashauri mahakamani.

Hivyo amewataka watumishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutoa haki kwa wakati kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika sekta hiyo.

Kazungu alitoa kauli hiyo juzi kwenye hafla ya kufungua jengo jipya la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mkoani Shinyanga, sambamba na ufunguzi wa majengo mengine matano kutoka mikoa ya Pwani, Manyara, Katavi, Rukwa na Shinyanga.

Alisema utoaji wa haki jinai kwa usawa na kwa wakati ni kupunguza malalamiko kwa jamii, hivyo watumishi kutoka ofisi za taifa za mashtaka wanapaswa kuzingatia maadili na weledi mkubwa katika utendaji wao kazi katika mnyororo wa haki jinai.

Aliitaka ofisi hiyo kuendelea kuweka mikakati ya kukamilisha ujenzi wa ofisi katika mikoa na wilaya zilizobaki, sambamba na kufanya maboresho kwenye maeneo mengine kama vile maslahi ya watumishi, pamoja na kuendelea kushirikiana na vyombo na taasisi zilizopo kwenye mnyororo wa utoaji wa haki jinai.

Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka nchini, Sylvester Mwakitalu, alisema baadhi ya mikoa na wilaya wameshajenga ofisi za taifa za mashtaka na mikoa mingine wamepanga ofisi na kwamba mwaka wa fedha ujao wametengewa fedha za maendeleo ambazo watazitumia kujenga ofisi tatu.

"Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inapaswa kuwa na majengo ya ofisi 169 katika mikoa na wilaya zote nchini, hadi sasa ofisi ina majengo sana ambayo yapo katika mikoa ya Iringa, Ilala-Pwani, Manyara, Katavi, Rukwa na Wilaya ya Serengeti, na tuna upungufu wa majengo 161," alisema Mwakitalu.

Naye Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, Frank Mahimbali, alisema kupitia ofisi hiyo mpya wanategemea ufanisi wa kazi utaongezeka pamoja na kupata hadithi nzuri za mashtaka mahakamani zisizo na ukakasi, huku akiomba ofisi kama hiyo ijengwe pia na Mkoa wa Simiyu.

Naye Mshauri Mwelekezi wa ujenzi wa ofisi hiyo, Israel Masawe, akisoma taarifa ya ujenzi huo alisema ulianza Oktoba 5, 2022, na umekamilika Machi mwaka huu kwa gharama ya Sh.bilioni 2.1.

# Deni la bil.7/- lakwamisha ukamilishaji ujenzi wa vivuko

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeiagiza serikali kumlipa mkandarasi Songoro Marine Transport Ltd Sh.bilioni saba anazodai ili akamilishe ujenzi wa vivuko.

Akizungumza juzi baada ya kamati hiyo kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa mkandarasi huyo, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Selemani Kakoso alisema wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa wanauhitaji wa vivuko hivyo.

Hivyo, aliamwagiza Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, kuhakikisha anapeleka fedha hizo kwenye huo mradi ili uweze kukamilishwa kwa wakati na kutowarudisha nyuma makandarasi wazawa katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Hapa angekuwa mkandarasi kutoka nje ya nchi lazima mngemlipa riba lakini kwa kuwa ni mkandarasi mzawa bado na yeye anahitaji kuendelea kukua ataishi kwa maumivu makali anaogopa akiwadai kwa kulazimisha mtamnyima tenda, ndicho kinachowaua wazawa," alisema Kakoso.

Baada ya maagizo hayo, Waziri Bashungwa aliahidi kufuatilia suala hilo baada ya ziara hiyo ambapo alisema ataenda kuweka kambi hazina kwa ajili ya kumuomba Waziri wa Fedha na wataalamu wake kulizingatia hitaji kubwa la mkandarasi huyo kulipwa fedha hizo ili wananchi waweze kupata huduma baada ya miradi hiyo kukamilika.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala, akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa kivuko kipya na maegesho ya Buyagu-Mbalika alisema kivuko hicho chenye urefu wa mita 30.25, upana mita 9.75 kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 50, abiria 100 na magari madogo sita.

Alisema mpaka sasa mradi huo umefikia asilimia 45.9 na umeongezwa muda kwa miezi minne bila ongezeko la gharama kutokana na kuchelewa kwa malipo baada ya kuwasilisha hati za madai.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songoro Marine Transport, Meja Songoro alisema tatizo walilokutana nalo ni kuchelewa kwa malipo ambapo mpaka sasa zaidi ya Sh.bilioni Saba.

"Katika karakana yetu ya Mwanza tunatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo Rugezi - Kisorya ambao umefikia asilimia 81, Ijinga - Kahangala asilimia 84, Bwiro - Bukondo asilimia 85, Nyakalilo- Kome asilimia 60 na Buyagu - Mbalika asilimia 45.9," alisema Songoro.




Mkurugenzi Mtendaji wa TANROAD, Mhandisi Mohamed Besta (kushoto), akibadilisha mkataba wa ujenzi wa barabara ya Kahama-Kakola yenye kilometa 73 na Mwakilishi wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), Liu Zenglong, itakayojengwa kwa Sh.bilioni 101.2, hafla iliyofanyiwa viwanja vya Shule ya Msingi Kakola Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Bil.101/- kutekeleza ujenzi barabara Kahama-Kakola

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imesaini mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Kahama-Kakola (Km 73) kwa kiwango cha lami itakayo gharimu Sh.bilioni 101.2 na kumaliza adha ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa eneo hilo.

Ujenzi wa barabara hiyo unatekelezwa na mkandarasi wa kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) ndani ya miezi 27 chini ya udhamini wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba huo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mohamed Besta, alisema ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na kuwa na viwango vinavyohitajika, utasimamiwa na serikali kupitia TANROADS.

Naye Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa alisema wakati mkandarasi huyo akiendelea na ujenzi serikali itaendelea kufanya upembuzi yakinifu katika kipande kilichobaki chenye kilometa 57.4 kutoka Ilogi hadi Mtakuja mkoani Geita, ili atakapomaliza ujenzi wa barabara hiyo ahamie kipande hicho na kuunganisha Mkoa wa Geita, Kahama, Mwanza na mikoa mingine.

Aidha, Bashungwa alisema serikali imedhamilia kukamilisha miradi yote ya barabara iliyokuwa imeanzishwa na Hayati Dk. Magufuli.

Alisema awali Daraja wa Kigongo-Busisi lilikuwa asilimia 25 ya utekelezaji wake na sasa umefikia asilimia 85 na litakapokamilika itafungua fursa za kiuchumi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

Mkazi wa Kijiji cha Kakola, Kata ya Bulyanhulu, Msanja Mezani ambaye ni mfanyabiashara wa madini alisema kwa sasa wanalazimika kusafirisha kaboni hadi Kahama Mjini kwenye uchenjuaji kwa Sh.250,000.

Alisema wakati mwingine wanakuwa na hofu ya kutekwa kwasababu ya ubovu wa barabara na sasa wamepata tumaini jipya baada ya kuanza ujenzi wake.

Naye Sakina Ngollo alisema wanapata changamoto katika kusafirisha mazao kutoka shambani hadi sokoni kwa sababu ya mazao yanaharibikia njiani husussani nyanya na matikiti maji na kupata hasara.

Nipashe Spotika



WACHEZAJI WANAOLIPWA MSHAHARA MKUBWA SAUDIA UK. 12

# MAKOCHA SABA WAOTAKIWA KUONEKANA EPL MSIMU UJAO



Xabi Alonso

**LONDON, England**

INAONEKANA kama msimu huu wa majira ya joto unaweza kushuhudia mabadiliko makubwa ya makocha kwenye Ligi Kuu ya England, EPL.

Kuondoka kwa Jurgen Klopp kutoka Liverpool kutafungua moja ya kazi kubwa zaidi duniani, huku Chelsea, Manchester United, Newcastle United na West Ham zikidokezwa kubadilisha mambo dimbani.

Kwa bahati nzuri, hakuna uhaba wa chaguzi zinazowezekana.

Hawa hapa ni makocha saba ambao wanatazamiwa kuonekana kwenye Ligi Kuu England msimu ujao...

**#7. RUBEN AMORIM**

Klabu nyingi za EPL zimekuwa zikifuatilia kwa karibu mafanikio ya Ruben Amorim akiwa na Sporting CP kwa miaka mingi sasa, lakini kwa sababu yoyote ile, hakuna aliyevuta hisia za kutaka kumnunua kocha huyo mwenye umri wa miaka 39.

Akiwa anaongoza soka la kuvutia na la werevu, Amorim mara kwa mara amekuwa akiongeza thamani ya wachezaji wake, na hivi karibuni zaidi akimgeuza Viktor Gyokeres kuwa mshambuliaji anayeweza kufunga mabao mengi.

Inahisiwa kama suala la muda kabla ya timu kama Chelsea, Liverpool au Manchester United kumchukua Amorim.

**#6. XABI ALONSO**

Liverpool wanataka Xabi Alonso kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp, na si vigumu kuona sababu. Kiungo huyo wa zamani ameigeuza Bayer Leverkusen kuwa timu isiyoweza kushindwa na yuko mbioni kuiangusha Bayern Munich msimu huu.

Ingawa mashabiki wengi wasioegemea upande wowote wanaweza kuwa na nia ya kumzuia kocha huyo aliyeibuka kutoka mikononi mwa Liverpool, kumwona Alonso akirejea Anfield kutamfanya kuwa mpinzani mkuu. Alichofanya Ujerumani kufikia sasa kimekuwa saa ya kuburudisha na tungependa kuona mengi zaidi kutoka kwake.

Hata hivyo, Bayern wanatazamia kuharibu furaha, huku Real Madrid wakitajwa kuwania saini yake kwa 2025.

**#5. ARNE SLOT**

Alianza kazi ya ukocha mnamo 2019, lakini tayari kuna mengi ya kupenda kuhusu bosi huyo wa Feyenoord.

Akipokea msukumo kutoka kwa Pep Guardiola - mbinu zake zote mbili na unyoaji wake wa nywele - Slot ameanzisha aina ya soka la kufurahisha kwa timu hiyo ya pale Rotterdam, na kuifanya timu yake kuwa 'jini' halisi walioshinda taji la 2022/23.

Kulikuwa na uhusiano na Tottenham Hotspur msimu uliopita wa majira ya joto, lakini baada ya Feyenoord kuchukua hatua ndogo nyuma msimu huu, lazima kuwe na timu nyingi za Uingereza ambazo zinaweza kumshawishi Slot kuhama.

**#4. JOSE MOURINHO**

Angalia, Jose Mourinho anaweza kuwa kocha maarufu zaidi kote, lakini bosi huyo wa zamani wa Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur ni sinema katika hali yake safi.

Kwa sasa akiwa huru tangu kuondoka kwake kutoka AS Roma, Mourinho anaweza kuwa na mafanikio makubwa kwa klabu yoyote iliyo tayari kumchukua. Uwezo wake wa kubeba mataji umefifia katika miaka ya hivi karibuni, lakini Mourinho bado ni kocha dhabiti ambaye uwapo wake kwenye Ligi Kuu England hautasaidia soka la Uingereza pekee.

**#3. HANSI FLICK**

Miezi 18 aliyoiongoza Bayern Munich ilijaa mataji na mafanikio makubwa, lakini mabadiliko ya Flick kwenye Timu ya Taifa ya Ujerumani hatimaye yaliishia kwa fedheha.

Barcelona ni miongoni mwa pande zinazovutiwa na Flick, ambaye bila shaka atazingatiwa na timu yoyote inayotafuta kocha mpya msimu huu wa majira ya joto.

**#2. ZINEDINE ZIDANE**

Imepita miaka mitatu mizima tangu Zinedine Zidane achukue kiti. Huu ni wakati mwingi wa kujua Kiingereza vizuri.

Vipindi viwili vyake akiwa na Real Madrid vilikuwa vya kufurahisha, lakini Zidane amekaa nyumbani kwa furaha akisubiri nafasi muafaka. Ikiwa ana kazi akilini, inaweza kuwa wakati wa kukubali kwamba inakuja Mannchester United.

Zidane ni mmoja wa watu wenye majina makubwa katika soka duniani, lakini hajawahi kupamba Ligi Kuu England kama mchezaji. Ni wakati wake muafaka wa kufanya jambo kuhusu hilo.

**#1. JULIAN NAGELSMANN**

Ilikuwa miaka minne tu iliyopita ambapo Julian Nagelsmann alikuwa kijana. Alikuwa mchanga, akizunguka-zunguka kwenye ubao wa kuteleza, alikunja miguu yake ya suruali na kuvaa viatu vya kupendeza siku ya mechi. Kila mtu alimtaka kwenye klabu yake.

Bayern Munich ilishinda kinyang'anyiro cha kuwania saini yake, lakini ilifanya uamuzi wa kushangaza kwamba ushindi wa mara 60 katika mechi 84 ulifanya mkataba usitishwe Machi 2023.

Ukweli kwamba alipewa kiatu hicho umeharibu sifa ya Nagelsmann, lakini si kwamba mambo yalienda kombo tu, kwani angalia mwelekeo wa Bayern tangu alipoondoka.

Mkataba wa Nagelsmann na Ujerumani unamalizika msimu huu wa majira ya joto. Ikiwa anataka mabadiliko ya mandhari, kusiwe na uhaba wa makocha kwenye Ligi Kuu.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya soka duniani kushinda jumla ya mechi 800 kwa klabu na nchi yake baada ya juzi kuiongoza Al Nassr kuibuka na ushindi wa mabao 4-3 dhidi ya Al-Ain. Katika ushindi huo wa mechi 800, mechi 316 alishinda akiwa na Real Madrid, 214 na Manchester United na 91 akiwa Juventus huku 125 ni akiwa na timu ya taifa.



## Extra Time



CRISTIANO RONALDO

# WACHEZAJI WANAOLIPWA MSHAHARA MKUBWA SAUDIA

**RIYADH, Saudi Arabia**

NIA ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, ya kuubadilisha mfumo wa sasa wa mpira wa miguu duniani imevutia baadhi ya majina makubwa kwenye ardhi yao.

Ujio wa Cristiano Ronaldo mwaka 2022 ulikuwa mapinduzi makubwa na si mshindi pekee wa zamani wa Ballon d'Or anayecheza Saudi Arabia, bali pia Karim Benzema anashiriki huko. N'Golo Kante naye yupo pale katika Klabu ya Al Ittihad.

Kwa wachezaji hawa, kushuka kwa ubora si muhimu sana kwao kutokana na kiasi kikubwa cha fedha ambacho klabu zimewapa. Mfuko wa Uwekezaji wa Umma - ambao unaisimamia pia Newcastle United - sasa unamiliki klabu kubwa nne za Saudi Arabia na fedha zitaendelea kuingizwa kwenye mradi huo.

Hawa ndio wachezaji tisa wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Saudia kwa sasa...

**#9. Marcelo Brozovic (Al Nassr)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni 403,000**

Marcelo Brozovic alicheza kwa kiwango cha juu sana msimu wa 2022/23 huku Croatia wakifurahia mchuano mwingine mkali kwenye Kombe la Dunia na Inter Milan walifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hiyo haikutosha kumbakisha Ulaya wakati Al Nassr walipopiga simu kumtaka.

Kiungo huyo alinunuliwa kwa euro milioni 18 na akaichezea timu yake mpya haraka kabla ya msimu mpya dhidi ya Inter, klabu ambayo hapo awali aliichezea mechi 330.

**#8. Kalidou Koulibaly (Al Hilal)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni 576,000**

Alikuwa na msimu mmoja tu pale Chelsea Kalidou Koulibaly, ambaye alikuwa mmoja wa mabeki bora wa kati barani Ulaya alipokuwa Napoli.

Kwa bahati mbaya kwake, Koulibaly alijiunga na 'Blues' katika msimu mbaya wa mpito wakati timu yake ya zamani ikitwaa taji la Serie A.

Baada ya kushindwa kuwa na ushawishi katika uwanja wa Stamford Bridge, Chelsea walikuwa na furaha zaidi kuwezesha kuondoka kwa Koulibaly huku wakipanga kujenga upya na kikosi cha vijana.

**#7. Sadio Mane (Al Nassr)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni 650,000**

Gwiji huyo wa Liverpool alistahimili kampeni mbaya akiwa na Bayern mara ya mwisho, na badala ya kubaki Ulaya, Mane alichagua utajiri wa Ghuba.

Die Roten walifurahia kumpoteza nyota huyo wa Senegal, huku Al Nassr wakimnasa kwa pauni milioni 24. Pia wamempa Mane mshahara mkubwa wenye thamani ya pauni milioni 34 kwa mwaka.

Mshambulizi huyo mwenye uwezo mwingi, ameungana na Cristiano Ronaldo mjini Riyadh, na maisha yake ya Saudia yameanza kwa kasi.

**#6. Fabinho (Al Ittihad)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni 692,000**

Mara moja katika kikosi cha Jurgen Klopp kwenye Uwanja wa Anfield, kudorora kwa Fabinho kulikuwa muhimu katika mapambano ya 'Wekundu' hao.

Liverpool wametafuta mapinduzi ya safu ya kiungo msimu huu na walifurahi kumruhusu Mbrazil huyo kuondoka kwenda Al Ittihad, ingawa bado hawajachukua nafasi ya kiungo mkabaji.

Mabingwa wa sasa wa Saudia Pro League wanaripotiwa kumpa Fabinho mshahara wa kila wiki wenye thamani ya karibu pauni kwa wiki 700,000.

**#5. Riyad Mahrez (Al Ahli)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni 865,000**

Riyad Mahrez alimaliza kipindi kigumu akiwa na Manchester City kama mshindi wa mataji matatu, baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England kule Leicester.

City walikuwa wamedhamiria kumbakisha nahodha huyo wa Algeria, lakini hali yake iliathiriwa na kutoshiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA na ofa kutoka kwa Al Ahli ilikubaliwa upesi.

**#4. N'Golo Kante (Al Ittihad)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni Mil 1.7**

N'Golo Kante hakuweza kuondoka Chelsea kwa shangwe nyingi, baada ya msimu mbaya uliotatizika katika kampeni yake ya mwisho pale Stamford Bridge.

Kiwango cha nyota huyo wa zamani wa Leicester katika miaka ya hivi karibuni hakikuwa kizuri na hivyo ofa ya Saudia ilikuwa bora kwake.

Kante alijiunga na Al Ittihad, ambao walifanya kazi kubwa ya kwanza katika dirisha la usajili la majira ya joto 2023.

**#3. Neymar (Al Hilal)**
**Mshahara wa kwa wiki: Pauni Mil 2.65**

Yote ilikuwa ya nini, eh? Mambo yote ya Neymar kwenda PSG, yaani Mbrazil huyo aliondoka katika mji mkuu wa Ufaransa akiwa ameshindwa kuwasukuma 'Les Parisiens' kufikia lengo lao kuu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akiwa na umri wa miaka 32, Neymar sasa anatamba huko Ghuba.

Haishangazi kwamba Mbrazil huyo anapokea mshahara mkubwa na Al Hilal.

**#2. Karim Benzema (Al Ittihad)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni Mil 3.58**

Mwaka mmoja baada ya kutwaa tuzo ya Ballon d'Or, Karim Benzema alichagua kuondoka Real Madrid na kuanza safari mpya Mashariki ya Kati.

Ingawa majeraha yalizuia msimu wake wa 2022/23, lakini Mfaransa huyo anashindana kwa kiwango cha juu zaidi akiwa pale Al Ittihad.

Benzema anaripotiwa kupata kiasi kinachokaribia rekodi ya Ronaldo ya mshahara wa pauni milioni 173 kwa mwaka.

**#1. Cristiano Ronaldo (Al Nassr)**
**Mshahara kwa wiki: Pauni Mil 3.6**

Baada ya kuondoka Manchester United kwa mara ya pili kiutata, Cristiano Ronaldo alikua kichwa kikuu cha kwanza cha Saudi Arabia alipotia saini mkataba mkubwa na Al Nassr wenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 173 kwa mwaka.

Mchezaji huyo bora wa muda wote walifurahia msimu mzuri wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Saudia, lakini mabao yake yalishindwa kuisaidia Al Nassr kutwaa ubingwa.

## Nukuu

"Nadhani Haaland ana furaha sana Manchester City kwa sasa, lakini tutaona. Natumai tunaweza kuona [Mbappe, Haaland, Bellingham] pamoja katika klabu moja. Itanikumbusha 'Galacticos', ikiwa wote wataishia Real Madrid," **Mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid, Mbrazil Ronaldo Nazario.**



"Inapendeza kuwa kileleni, hiyo ni hakika - nadhani ni hali ya kushangaza kwamba hata [sisi] tunahusika, tukiangalia kiwango ambacho timu hizo mbili [Liverpool na Manchester City] zinacho na bado tupo kileleni. Kwa hivyo, matarajio yanaongezeka, tunataka kuendelea kuwa pale, na lazima twende mchezo kwa mchezo," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, kuhusu mbio za ubingwa Ligi Kuu England.**



"Ni tofauti. Hii haimaanishi bora au mbaya zaidi. Kuna mbinu ndogo. Kwa kiwango cha kimbinu, La Liga ni bora zaidi kuliko ile ya Uingereza. Tukizungumzia kuhusu nguvu, kasi ama uimara, mdundo, Ligi ya Uingereza inaweza kuwa na zaidi. Lakini ya Kihispania ina ubora zaidi wa mbinu," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, akieleza tofauti za kiufundi kati La Liga (Ligi Kuu Hispania) na Premier League (Ligi Kuu England).**





Kikosi cha Simba ambacho kimeweka rekodi ya kuruhusu mabao mengi msimu huu, lakini pia kufungwa mechi nyingi tofauti na msimu uliopita.

# REKODI SABA MBAYA ZILIZOWEKWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

NI raundi 10 zimebaki kabla ya kukamilika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Bado hakuna rekodi nyingi nzuri zilizovunjwa mpaka sasa ukilinganisha na zile za msimu uliopita.

Klabu nyingi ikiwamo Simba, Yanga na Azam, hazijavunja rekodi zao nzuri za matokeo na takwimu ambazo ziliziweka msimu uliopita.

Hata hivyo, Yanga na Azam pia bado hazijaweka rekodi mbaya mpaka sasa ukilinganisha na za msimu uliopita.

Simba na baadhi ya timu za Ligi Kuu zimeanza kuweka rekodi ambazo si nzuri ukilinganisha na zile ambazo zilizipata msimu uliopita.

Katika makala haya, tumekusanya baadhi ya rekodi mbaya za matokeo na takwimu zilizowekwa mpaka sasa wakati ligi ikielekea ukingoni.

### Simba yaruhusu mabao mengi msimu huu

Kabla ya Ligi Kuu kumalizika, tayari Simba imeruhusu mabao 18 kwenye wavu wake ikiwa ni rekodi mbaya ukilinganisha na ya msimu uliopita.

Simba imecheza mechi 19 mpaka sasa, lakini imeruhusu wavu wake kugushwa mara 18, ikiwa ni karibu wastani wa bao moja kila mechi.

Msimu uliopita hadi inamaliza ligi, ikicheza mechi 30, ilikuwa imeruhusu mabao 17, hivyo ina bao moja zaidi ya idadi ya yale iliyofungwa msimu uliopita.

### KMC mwendo wa sare

Timu ya KMC mpaka sasa inaongoza ikiwa na sare nyingi (10) kwenye Ligi Kuu. Imepata sare hizo kwa mechi 21 ilizocheza, ikifuatiwa na Tabora United, ambayo inazo tisa.

KMC imevunja rekodi yake ya msimu uliopita, ambapo mpaka inacheza mechi 30 na kumaliza ligi ilimaliza na sare nane tu.

### Simba yafungwa mara mbili

Msimu uliopita Simba ilimaliza mechi 30 ikiwa imefungwa mechi moja tu. Mechi iliyopoteza ilikuwa ni dhidi ya Azam FC, ikifungwa bao 1-0, Oktoba 22, 2022, lakini msimu huu mpaka sasa imepoteza mechi mbili.

Ilifungwa mabao 5-1, Novemba 5, mwaka jana, dhidi ya Yanga, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Machi 6, mwaka huu, ilipoteza kwa mabao 2-1 msimu huu dhidi ya Prisons.

### Kagera msimu huu siyo

Timu ya Kagera Sugar imevunja rekodi ya sare zake za msimu uliopita ikiwa imecheza michezo 21 tu. Ina sare tisa ikishika nafasi ya pili kwa timu zenye sare nyingi Ligi Kuu, rekodi zikionyesha kuwa mpaka inamaliza ligi msimu uliopita, ikicheza mechi 30 ilikuwa na na sare nane tu.

### Singida mwaka wa shetani

Singida Fountaine Gate imepoteza michezo tisa mpaka sasa ikiwa ni ongezeko la mechi mbili mpaka ilipomaliza mechi zake za ligi msimu uliopita.

Timu hiyo ambayo imeshacheza mechi 20, imepoteza idadi hiyo ya mechi, huku mechi 30 za msimu uliopita ilikuwa imepoteza michezo saba tu.

### Namungo nayo haijakaa vema

Timu ya Namungo FC nayo imetoka sare nane mpaka sasa ikiwa imeshacheza michezo 20, ikivunja rekodi ya zile ambazo ilikuwa nazo msimu uliopita. Mpaka inamaliza msimu uliopita ilikuwa na sare saba, hivyo mpaka sasa ina ongezeko ya sare moja.

### Ihefu bado yajitafuta

Wakati ikidhaniwa kuwa msimu huu iko vizuri zaidi kuliko uliopita, rekodi zinakataa. Ihefu FC ina sare nyingi zaidi msimu huu kuliko uliopita. Imetoa sare tano mpaka sasa ikicheza mechi 20 ligi. Rekodi zinaonyesha kuwa msimu uliopita ilitoa sare tatu tu, hivyo kuvunja rekodi ya msimu uliopita, ikiwa ni ongezeko la sare mbili mpaka sasa.

## JE, WAJUA?




BAO alilofunga wakati Bayern ikishinda 5-2 ugenini juzi dhidi ya Darmstadt, linamfanya Harry Kane kufikisha mabao 31 hadi sasa msimu huu na hivyo kuweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Bundesliga kufunga mabao mengi zaidi katika msimu wake wa kwanza kwenye ligi hiyo, akiivunja ile ya Uwe Seeler ya mabao 30 akiitumikia Hamburg msimu wa 1963-64.





Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira wa Jiji la Dodoma, Dikson Kimaro (kulia), akishirikiana na wakazi wa Mtaa wa Chidachi kusafisha mtaro wa kupitisha maji kandokando ya barabara ya kutoka Kikuyu hadi St Mary jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Familia zalala nje dalali akifunga nyumba

**Na Halfani Chusi**

MVUA kubwa inanyesha Dar es Salaam, lakini familia mbili katika Kata ya Ndugumbi, wilayani Kinondoni zinalala nje kutokana na dalali wa mahakama kufunga nyumba zao.

Tangu Ijumaa familia za Juma Kanyoni na Jamila Tamimu zimelazimika kulala nje ya nyumba zao baada ya kampuni ya udalali Yono Auction Mart kutoa vyombo vyao nje kutekeleza agizo la mahakama.

Vyombo vya familia hizo vilitolewa makazi yao na kampuni hiyo chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi kisha nyumba hizo kufungwa, huku wakuu wa kaya hizo wakidai wameishi katika eneo hilo kwa zaidi ya miaka 15 na wanashangaa kutakiwa kupisha.

Jamila alidai wamekuwa na kesi kuhusu nyumba hizo kwa muda mrefu na jirani yao, Emmanuel Mbilinge anayedai hilo ni eneo lake tangu mwaka 1982.

Huku akishindwa kuzuia machozi yake, Jamila, akiwa nje ya nyumba aliyofukuzwa, alidai ameishi hapo kwa miaka 38 sasa, alinunua eneo hilo na hata hati na nyaraka zote za ununuzi anazo.

"Kesi ya mgogoro huu ni ya siku nyingi, juzi ilikuwa siku ya kwenda mahakamani, lakini Yono Auction Mart pamoja na Askari wa Jeshi la Polisi walifika hapa saa 6:30 mchana wakaanza kutoa vyombo kwa jirani yangu (Juma Konyani), baadaye wakahamia kwangu.

"Wakaniuliza 'haujui kama kuna agizo hapa mnatakiwa kuhama?' Nikawaambia 'sawa lakini kesi bado iko mahakamani inaendelea, kwanini tusisubiri uamuzi utakaotolewa?'

"Muda kidogo jirani yangu akafika kutoka mahakamani na hati ya zuio (stop oder), nikawaambia kibali hiki hapa cha kuzuia kisifanyike chochote kimefika, wakasema 'tutajuaje kama ni feki? Wakaendelea kutoa vyombo nje, wakafunga milango na makufuli yao mpaka sasa tupo nje hapa hatujui twende wapi," alilalama mama huyo.

Naye Juma Konyani alidai amekaa katika nyumba iliyofungwa na dalali tangu mwaka 2008 na ana hati ya umiliki na anashangaa wakati yuko mahakamani, alipata taarifa kuna watu wanatoa vyombo nyumbani kwake.

"Tunaomba serikali itusaidie, tulishinda kesi katika Mahakama ya (Hakimu Mkazi) Kisutu, kuna mwekezaji anataka kuchukua hii sehemu ndio maana tunapitia katika wakati huu mgumu," alidai.

Alionesha hati ya zuio (stop order) aliyodai kupewa na mahakama kwa ajili ya kuzuia lisifanyike jambo lolote kwenye nyumba hiyo, lakini licha ya kuwaonesha, dalali aliendelea kutoa vyombo ndani ya nyumba hiyo.

Alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi, mlalamikiwa Emmanuel Mbilinge, alidai hilo ni eneo; alilinunua mwaka 1982 kwa mtu aliyemtambulisha kwa jina la Saidi Rashidi, lakini baadaye mwaka 1988 Jamila Tamimu ambaye ni jirani yake "alitapeliwa na kuuziwa tena na mwuzaji (Rashid)".

Alidai kuwa mwaka 2008 walimtapeli tena Juma Konyani kwa kumwuzia eneo hilo hilo mbele yake, akisisitiza kwamba walitapeliwa bila kujua kwamba eneo hilo ni lake tangu mwaka 1982.

"Baada ya hapo kesi ikaanza kunguruma Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Mwaka jana mwezi wa kumi (Oktoba) nilishinda kesi. Kwa hiyo, kilichofanyika juzi nilikuwa ninakazia hukumu yangu ya kuwataka wahame.

"Wote tumeuziwa na Saidi Rashidi ambaye alishafariki dunia. Huyo ndiye aliwatapeli, aliwauzia eneo ambalo tayari alikuwa ameniuzia mimi," alidai.

Alipoulizwa kuhusu zuio la mahakama 'stop order' lililotolewa na mahakama, Mbilinge alidai hakuliona wala hakuoneshwa kabla ya kuanza kutoa vyombo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ulioko mgogoro huo, Yusuph Debe alisema anafahamu eneo hilo lina mgogoro wa muda mrefu, lakini hakuwa na taarifa za kampuni ya udalali Yono Auction Mart kufika eneo hilo kutoa vyombo na kufunga milango.

Dalali wa Mahakama kupitia kampuni ya Yono Auction Mart, Stanley Kevela alithibitisha kutoa vyombo vya walalamikaji hao, akidai ni utekelezaji wa agizo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

"Ilitakiwa kama alikuwa na hati ya zuio (stop oder) alete mapema ofisini kwetu, angefanya hivyo mapema wala tusingevamia, hakuna mtu anaweza kupingana na uamuzi wa mahakama.

"Ninachoelewa hao walishindanishwa kwenye mahakama wakashindwa, walikwenda mpaka Mahakama Kuu wakashindwa, hata polisi wenyewe wasingeweza kusimamia bila kuwa na uhakika.

"Hata Mkuu wa Wilaya Kinondoni, Saad Mtambule alitoa baraka zote, tulikuwa tunakamilisha uamuzi wa mahakama, yule alikuwa amezungushwa zaidi ya miaka sita, sisi tulitekeleza amri ya mahakama," alidai.

# Ujangili wa tembo wapungua

**Na Jenifer Gilla**

UJANGILI wa tembo umepungua nchini kutoka matukio 18 yaliyoripotiwa mwaka 2016 hadi matatu yaliyoripotiwa mwaka jana, hivyo kusababisha kuongezeka kwa wanyamapori hao.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imesema hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarishwa ulinzi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na ushirikishwaji jamii katika mambo ya uhifadhi.

Kwa mujibu wa takwimu za serikali zilizotolewa Juni 2015, idadi ya tembo nchini ilipungua kutoka 109,051 mwaka 2009 hadi kufikia 43,330 mwaka 2014, hali ambayo ni tofauti na sasa; idadi imeongezeka hadi nchi kuwa na zaidi ya tembo 60,000 mwaka 2019.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uhifadhi Kitengo cha Uchunguzi wa TAWA, Tryphone Kanoni kwa waandishi wa habari wanachama Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) wilayani Bagamoyo, akionesha kuwa biashara ya nyara za tembo zimepungua kwa kiasi kikubwa.

"Kwa sasa biashara ya meno ya tembo nchini kwetu imekwisha, hata matukio ya ujangili wa tembo ni kama vile yamekwisha, tofauti na ilivyokuwa huko nyuma," alisema Kanoni.

Alisema walipima matokeo hayo kwa kupungua kwa mizoga ya tembo waliouawa na majangili kwenye maeneo mengi ya hifadhi nchini. Awali mizoga hiyo ilikuwa mingi kulinganisha na sasa.

Kwa mujibu wa Kanoni, hata meno ya tembo yanayokamatwa kwa sasa mengi ni ya miaka ya nyuma; mapya yamekuwa nadra kuonekana, jambo ambalo linaonesha mapambano dhidi ya ujangili yanazaa matunda.

Alisema pamoja na matokeo hayo, mamlaka hiyo imeongeza kasi ya ulinzi kwa kutumia teknolojia mbalimbali za kisasa, ili kudhibiti majangili na kuokoa wanyamapori wengine kutoka kwenye dhahama hiyo.

Ofisa huyo alisema pia wanadhibiti mitandao inayofanya biashara hiyo kupitia mitandao ya kijamii kwa kuwa ripoti inaonesha Tanzania ni moja ya nchi zinazotumia njia hiyo kama mawasiliano ya uhalifu wa wanyamapori.

Katika operesheni hizo, alisema mamlaka hiyo ilifanikiwa kukamata washukiwa wa mauaji ya tembo 3,700 mwaka 2023 kulinganisha na 4,800 walioripotiwa kufanya ukatili huo mwaka 2016.

Meneja Ushirikishwaji Sekta Binafsi Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, Dk. Elikana Kalumanga, alisema kupungua kwa ujangili wa tembo kumetokana na nguvu ya pamoja kati ya serikali na sekta binafsi.

Alisema kupitia miradi ya kuelimisha na kuwezeshwa kiuchumi, jamii imetambua faida ya maeneo ya hifadhi, hivyo kushiriki katika kuyalinda ili iendelee kunufaika na fursa zitokanazo na kuwapo wanyamapori hao karibu na makazi yao.

"Kupitia Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili tumeona fursa kama biashara, uhifadhi, kilimo, ufugaji wa nyuki na jamii husika kuaminika katika taasisi za kifedha, jambo ambalo awali halikuwapo," alisema.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC), Abdallah Katunzi alisema ili kutokomeza ujangili wa wanyamapori nchini, kunahitaji nguvu ya pamoja kati ya serikali, sekta binafsi na vyombo vya habari.

Alishauri waandishi wa habari kujikita katika uandishi wa uhifadhi ili kuandika habari zenye tija na kuleta mabadiliko chanya katika jamii hasa zinazoishi karibu na hifadhi.

"Ninawashauri waandishi wa habari kubobea katika uandishi wa habari za uhifadhi, mazingira na wanyamapori, kwani ni eneo muhimu katika uendelevu wa nchi, lakini pia hata ujangili utadhibitika," alisema Katunzi.



# Bil.10/- kumaliza tatizo ukosefu wa maji Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya WSSA), imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi miwili ya maji inayotarajiwa kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji katika Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Barnabas Konga, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya wahandisi wa habari ya kutembelea baadhi ya vyanzo vya maji vinavyosimamiwa na mamlaka hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Maji Duniani.

Konga aliitaja miradi inayotekelezwa kuwa ni Mradi wa Chanzo cha Maji cha Mwasekwa ambacho kinatarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 40,000 wa kata tatu za jiji hilo na Mradi wa Maji wa Ilunga ambao unatarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 100,000 wa Mji wa Mbalizi na baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya.

Konga alisema mradi wa Mwasekwa unagharimu Sh. bilioni 5.2 na wa Ilunga unagharimu Sh. bilioni 4.8 na kwamba miradi hiyo ni kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji katika kipindi cha mwaka mmoja.

"Mahitaji ya maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi ni lita za ujazo milioni 90 lakini kwa sasa uzalishaji ni lita za ujazo milioni 66.5, kwa hiyo ili kufikia lengo ndiyo maana tunatekeleza miradi hiyo ya muda mfupi wakati tukisubiri mradi wa chanzo cha Mto Kiwira," alisema Konga.

Alisema tatizo linaloikabili mamlaka hiyo na kusababisha kuwa na upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo ni upotevu wa maji unaotokana na kupasuka kwa mabomba yaliyochakaa, uunganishaji wa maji holela unaofanywa na baadhi ya wananchi pamoja na ujenzi wa barabara.

Meneja wa Uendelezaji wa Miundombinu wa Mbeya-WSSA, Deogratius Leonidas ambaye anasimamia utekelezaji wa mradi wa Mwasekwa alisema mradi huo umekamilika kwa zaidi ya asilimia 70 na kwamba wananchi tayari wameanza kupata huduma.

Alisema wameshakamilisha ujenzi wa chanzo pamoja na eneo la kusafishia maji na kwamba kilichobakia kwa sasa ni ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji ambalo alisema wanatarajia kulikamilisha kabla ya Juni mwaka huu.

Alisema kwa sasa wanazalisha maji kutoka kwenye chanzo na kwenda moja kwa moja kwa wananchi, jambo ambalo alisema limesaidia kupunguza shida kwa wananchi wa maeneo yanayolengwa.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo husika ili waunganishiwe huduma hiyo na kwamba mpaka sasa wana maombi zaidi ya 100 ya wananchi wanaotaka kuunganishiwa.

Naye Meneja wa Mradi wa Ilunga, Uswege Mwaipopo alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 98 na kwamba kazi zilizobakia kwa sasa ni umaliziaji wa baadhi ya maeneo machache yaliyobaki.

Alisema kwa sasa eneo kubwa wanaloendelea na ujenzi ni la kusafishia na kutibia maji na kwamba maji tayari yameshafika kwa wananchi kutokana na mradi huo kusafirisha maji kwa njia ya mseleleko.



Mafundi wanaotekeleza mradi wa maji wa Iunga katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya wakiunganisha mabomba makubwa juzi kwa ajili ya kusafirisha maji kutoka kwenye eneo la kusafishia kwenda kwa wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Malezi, makuzi mabovu chanzo ongezeko la VVU

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MALEZI na makuzi yasiyofaa kwa watoto imetajwa kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko la maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa wasichana rika balehe na vijana.

Hayo yalielezwa wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa vya kisasa, kuwawezesha wasichana rika balehe na wanawake vijana kujikwamua kiuchumi.

Vifaa vilivyokabidhwa ni vyerehani vya kutengeneza nguo na viatu, mashine ya kukamulia mafuta ya alizeti na sabuni.

Vifaa hivyo vimetolewa na Shirika la HJF Medical Research International kupitia mradi wa dreams unaofadhiliwa na Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR) ya Idara ya Ulinzi ya Marekani (DOD), unaofanya kazi chini ya mfuko wa PEPFAR. Dorcus Binala(23) kutoka Kijiji cha Masebe Kata ya Mwaya wilayani Kyela ambaye ni miongoni mwa wasichana waliojiingiza kwenye tabia hatarishi ya ukahaba kwa sababu ya maisha duni katika familia yao alitoa ushuhuda katika hafla hiyo.

Dorcus alisema maisha duni yalisababisha kujiingiza kwenye ukahaba na hatimaye akapata ujauzito na mwanaume aliyempatia kukataa kutokana na tabia alizokuwa nazo.

"Leo ninaonekana ni binti mwenye nyuso ya furaha mbele yenu ni kwa sababu ya kunufaika na mradi wa dreams, nashukuru sana wafadhili wa huu mradi kwa kubadilisha historia ya maisha yangu kutoka kwenye tabia hatarishi za ngono ili kujipatia riziki na kuwa binti ninayefanya kazi njema kujiingizia kipato, lakini kuwa balozi katika mapambano ya virusi vya Ukimwi," alisema Dorcus.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi wa Shirika la HJF Medical Research International, Sally Chalamila, alisema vifaa hivyo vina thamani ya Sh. milioni 178 na kwamba vitasaidia kubadilisha maisha yao kwa kujikwamua kiuchumi na kukinga na kumpambana na maambukizi ya VVU.

"Tangu kuanza kwa mradi huu wa dreams mkoani Mbeya mwaka 2016 mabinti 130,000 wamefikiwa wakiwamo wa Wilaya ya Kyela, bado tunaendelea na kazi hii ya kuhakikisha tunatokomeza maambukizi mapya ya VVU, kutoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa na kuwawezesha mabinti kujikwamua kiuchumi," alisema Sally.

Mtaalam wa masuala ya kuzuia maambukizi ya VVU ambaye ni mwakilishi kutoka WRAIR/DOD, Dk. Alick Kayange alisema idadi ya watu wanaotambua hali zao imeongezeka kutoka asilimia 55.7 mwaka 2016/2017 hadi 87.4 ya mwaka 2022/2023.

Alkisema licha ya mafanikio hayo lakini bado kuna kazi ya kuhakikisha malengo ya sifuri tatu yanafikiwa ifikapo mwaka 2030, ili kusiwe na maambukizi mapya ya VVU wala vifo vitokanavyo na Ukimwi na unyanyapaa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenister Mhagama ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jafary Haniu aliwataka vijana wa kike na kiume kusimama katika maadili mazuri.

Alisema vikwazo vya kifedha na mazingira visiwe sababu ya kuwaingiza katika mitego ya maadili yasiyofaa.

Alisema mradi wa dreams umewanasua mabinti wengi wenye umri wa miaka 15 hadi 24, ambao walikuwa katika hatari kupata maambukizi ya VVU.

Aliongeza serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa mashirika hayo katika kudhibiti maambukizi ya VVU katika halmashauri zote zinazotekeleza mradi ikiwamo Kyela, Mbarali na Jiji la Mbeya.

# Naibu Waziri awatangazia neema wakazi Kijiji cha Luvuyo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wanaoishi jirani na chanzo cha maji cha Igongwi kilichopo katika Kijiji cha Luvuyo, Kata ya Madope wilayani Ludewa mkoani Njombe, wamehakikishiwa kuwa wa kwanza kupata huduma ya majisafi na salama, kabla hayajasambazwa katika maeneo mengine ya mkoa huo.

Ahadi hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira mkoani hapa iliyolenga kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maji, katika vijiji vya Luvuyo, Kitulila, Madobole, Luponde na Njomlole.

"Kijiji ambacho kinatunza chanzo cha maji lazima kiwe cha kwanza kunufaika kupata maji safi na salama ndipo yapelekwe kwa majirani zao," alisema Mahundi.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa vipande ambapo kukamilika kwake kunatarajia kunufaisha wananchi zaidi ya 9,000.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Jackson Kiswaga aliipongeza wizara ya maji kwa usimamizi mzuri wa utekelezaji wa miradi maji.

"Lakini tumesikia malalamiko yenu kwamba mradi huu umekaa muda mrefu na mngependa umalizike, tumekuja hapa kama kamati tuwasikilize tuisikilize wizara lakini tuweke mkakati wa pamoja ni namna gani tunakwenda kutatua changamoto ambazo zipo," alisema Kiswaga.

Awali Meneja wa Wakala wa Maji na usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Njombe, Sadick Chaka alisema mwaka 2023 hadi 2024 miradi 29 inaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali vijijini.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema viongozi wapo tayari kusimamia miradi ya maji lengo ikiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo bila ya changamoto.





# Waliobadilisha matumizi nyumba za serikali waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imewataka wananchi wanaopewa nyumba za maendeleo kwa ajili ya makazi kuacha tabia ya kubadilisha matumizi.

Naibu Waziri, Wizara hiyo, Salha Mohammed Mwinjuma, alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kutembelea nyumba za maendeleo zilizopo Mombasa Kwamchina zinazosimamiwa na Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC).

Alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kuzibadilisha matumizi nyumba hizo kitendo ambacho ni kosa na hakikubaliki kwa mujibu wa sheria.

"Hali ambayo tunakwenda nayo kwa sasa tunahisi kuna baadhi ya wananchi wameanza kukiuka matumizi ya nyumba hizi na tumejionea wenyewe zipo nyumba zimebadilishwa matumizi kwa kukatwa kuta zake kuanzia juu hadi chini", alisema.

Akizungumzia nyumba moja iliyobadilishwa matumizi yake, Salha alisema serikali inaifungia nyumba hiyo na kwamba hakuna shughuli itakayoendelea kwa sasa.

Alisema kuwa serikali itachukua hatua kali kwa mwananchi aliyepewa nyumba hiyo, kwani amekiuka masharti aliyopewa.

Alisema serikali imetoa nyumba hizo kwa mapenzi kama walivyokwenda kuomba kushirikiana katika kuziweka safi na nyumba nyingi zilizopo katika eneo hilo mazingira yake hayaridhishi.

Hivyo alisema kwamba serikali itahakikisha inazipitia nyumba zote ili kujiridhisha, kuona yale yote waliyokubaliana na wananchi katika mkataba wa ukodishwaji wa nyumba hizo yanatekelezwa kwa ufanisi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZHC, Mwanaisha Ali Said, alisema walifanya ukaguzi katika nyumba hizo na kugundua nyumba moja imefanyiwa uharibifu na mpangaji kwa kuvunja kuta ambazo zinashika nyumba yenyewe kwa kutaka kubadilisha mwonekano wa ndani.

"Inaonekana kwamba amechanganya vyumba viwili anataka kufanya chumba na choo na mwonekano wa nyumba hizi za maendeleo hazikujengwa hivyo hilo ni kosa," alisema.

Alisema kuwa uharibifu kama huo uliofanywa ni tatizo kubwa kwa nyumba zote za maendeleo ikiwamo Michenzani, Kiwajuni na Kilimani na mara nyingi wanapofanya ukaguzi wamekuwa wakikutana na changamoto hiyo.

Mwanaisha alisema shirika limepanga kumshtaki mpangaji huyo aliyefanya uharibifu huo, kwamba shirika limekuwa likikemea mara kwa mara tabia ya kurekebisha mwonekeno wa nyumba, pamoja na kukemea tabia ya kuvunjwa.

"Tumekuwa tukitoa elimu na matangazo lakini bado tatizo hili linaendelea kwa sababu inaonesha hatuchukui hatua kali sasa tumeazimia kuchukua hatua za kisheria zaidi kwa kumshtaki mmiliki wetu huyu na wengine ambao wanakiuka sheria zetu," alisisitiza. Mwanasheria wa ZHC, Yunus Juma Ali, alisea watahakikisha wanakwenda katika hatua za kisheria zaidi kwani tayari mpangaji huyo amekwenda kinyume na mkataba alioingia kati yake na serikali kupitia shirika hilo.

Alisema kuwa Kifungu Namba 3 cha mkataba huo kinaeleza wazi matumizi ya nyumba hizo, kwamba mpangaji huyo amekwenda kinyume kwa matumizi mengine.

Alisema lakini mpangaji huyo pia amejaribu kuuza au kumkodisha mtu mwingine jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 32 cha Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014 ya Sheria ya ZHC.

# Serikali kuanza kugawa vitalu vya mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar inatarajia kutangaza ufunguzi wa ugawaji wa vitalu vya mafuta na gesi, kwamba hafla hiyo inatarajiwa kufunguliwa na Rais Hussein Ali Mwinyi, Machi 20 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shabani Othman, alisema sambamba na ugawaji wa vitalu, Serikali ya Zanzibari ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Mafuta na Gesi ya Asilia Namba 6 ya mwaka 2016.

Alisema lengo ni kuimarisha mazingira bora ya uwekezaji katika utafutaji, uchimbaji na uendelezaji wa mafuta ya gesi asilia ili kuwavutia wawekezaji.

"Nikiwa waziri mwenye dhamana ya mafuta na gesi asilia kwa Zanzibar, nina furaha kubwa kuwajulisha rasmi kwamba maandalizi yote husika yanayohitajika ili Zanzibar kuweza kuanza kutoa vitalu kwa wawekezaji kwa ajili ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia yamekamilika," alisema waziri huyo.

Aidha, alisema Zanzibar ipo tayari kutangaza duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu katika maeneo ya baharini kwa wawekezaji wa mafuta na gesi asilia.

Waziri huyo alitoa pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa hatua hiyo kubwa na ya kihistoria kwa maendeleo ya nchi.

Alisema hatua hiyo ya duru ya kwanza ya utangazaji wa vitalu itafungua fursa za uwekezaji zitakazopelekea kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar na kuiweka katika ramani ya dunia kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia.

Hata hivyo alisema mafanikio hayo yasingeweza kufikiwa bila ya uongozi wake imara na madhubuti, pamoja na miongozo yake anayoitoa kwa viongozi.

Hivyo, alizitaka kampuni za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kote duniani, kushiriki katika duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya mafuta na gesi asilia kwa maeneo ya baharini.

Alisema: "Napenda kuwahakikishia wawekezaji wote kwamba Zanzibar iko tayari kuwapokea na kushirikiana nao katika kuendeleza sekta hii ya mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar".



Mkuu wa Uendeshaji wa Matawi ya Benki ya Absa Tanzania, Mwilongo Irene Msungu (kushoto), akipokea tuzo ya shukurani kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, kwa kutambua mchango wa Absa kama mdhamini mkuu katika uzinduzi wa Chama cha Wanawake Sekta ya Fedha Tanzania (TAWiFA), wakati wa hafla iliyofanyika Kizimkazi, Zanzibar jana, mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika Zubeir ahimiza uhusiano wa biashara unaoheshimu imani za dini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, amehimiza mashirika, taasisi na biashara binafsi kutambua umuhimu wa kukuza uhusiano wa kibiashara na utoaji huduma unaoheshimu na kudumisha maadili na imani za kidini za wateja na wadau wao.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipohudhuria na kuongoza futari iliyoandaliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) mahususi kwa wateja wake wa Kiislamu visiwani hapa. Hatua hiyo ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo kuandaa hafla za namna hiyo maeneo mbalimbali nchini, ikilenga kuonesha mshikamano na umoja katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyohudhuriwa na wageni mbalimbali waalikwa, wakiwamo viongozi waandamizi serikalini, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wabunge na wateja wa benki hiyo, Spika Zubeir alisema uhusiano wa kiimani kati ya mtoa huduma na mpokea huduma husaidia kutengeneza muunganiko imara wenye tija kubwa baina ya pande hizo mbili.

"Mashirika na taasisi nyingine zinapaswa kuendelea kuliona hili kama mfano wa kuigwa kutoka NBC na wadau wengine wanaotumia utaratibu huu kuonesha jinsi biashara inavyoweza kushirikiana vizuri na wateja wao na kuheshimu tamaduni na dini zao.

"Kwa kuandaa matukio ya aina hii yanayogusa na kutambaa tamaduni na imani za wateja wake, NBC Bank inathibitisha azma yake ya kutoa huduma bora za kifedha na pia kukuza hisia ya kuwa na uhusiano na maadili yanayofanana kati ya wateja wake," alisema Spika Zubeir.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo Wadogo, La Riba na Wakulima kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, kwenye hafla hiyo alisisitiza umuhimu wa uhusiano mzuri kati ya benki na wadau wake muhimu ikiwamo serikali na wateja.

Zaidi Urassa aliangazia huduma maalum ya benki hiyo, "La Riba," iliyoandaliwa kwa ajili ya wateja wenye imani ya Kiislamu kwa kuzingatia kanuni za dini hiyo katika masuala yanayohusiana na fedha na mtazamo wako kwenye riba.

Katika tukio la hilo, wageni waalikwa walipata wasaa wa kuzungumza na kubadilishana mawazo na maofisa wa benki hiyo.

Kama njia ya kurejesha shukrani zake kwa wateja hao, benki hiyo ilitoa zawadi maalum kwa wote waliohudhuria wote ikiwa ni ishara ya dhamira ya benki ya kukuza uhusiano imara na kuonesha shukrani kwa ushirikiano unaendelea baina ya pande hizo mbili.

# NIRC: Miradi umwagiliaji kukamilika kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) imewahakikishia Watanzania inaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji nchini ukiwamo wa vijana wa Chinangali na Ndogowe iliyo chini ya Mpango wa Jenga Kesho Iliyobora kwa Vijana 'Building Better Tomorrow' (BBT); unaosimamiwa na Wizara ya Kilimo.

Akizungumza baada ya ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa, alisema katika mashamba ya BBT, NIRC imehakikisha ujenzi wa miundombinu ikiwamo mabwawa, visima na mashamba yanakamilika kwa wakati. Alisema hatua hiyo imekusudia kuunga mkono jitihada za serikali za kuimarisha sekta ya kilimo na kupata matokeo chanya katika miradi hiyo ikiwamo ajira kwa vijana na ukuaji pato la taifa kwa asilimia 10 ifikapo 2030.

"Miradi ya kilimo kwa vijana BBT, Chinangali na Ndogowe kazi inafanyika ambapo kwa upande wa Ndogowe ikiwa ni moja ya miradi ya BBT mkoani Dodoma unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 21.7; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tumehakikisha tunabadili mfumo wa umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya mabomba badala ya mifereji.

"Tumefanya ukaguzi wa kazi za mkandarasi kwa kuangalia mabomba hayo yanayotoka katika kiwanda na kwenda eneo la mradi ambayo yatawekwa katika kilomita 104 kuanzia bomba kubwa hadi madogo huku mkandarasi akiwa na wajibu wa kutengeneza kilomita 14 za barabarana, kilomita tano za kuingia shambani, ujenzi wa nyumba ya msimamizi wa shamba Pamoja na ujenzi wa madaraja madogo," alisema.

Mndolwa alisisitiza kuwa mkataba wa ujenzi huo umeanza mwaka jana na kumekuwa na changamoto ya mvua hali iliyosababisha mkandarasi kusimamisha shughuli za mradi kwa muda.

Aidha, Mkurugenzi Mndolwa alisisitiza kuwa tume inaendelea na ukamilishaji wa mradi wa Chinangali katika mashamba ya BBT kwa ajili ya mashamba ya vijana na ujenzi wa miundombinu ikiwamo mabwawa, visima na usafishaji wa mashamba unaendelea.

Alisisitiza kuwa miradi hiyo inakabiliwa na mvua hali inayochangia mitambo kuzama na matumaini ya tume ni kwa sasa wakati ambapo mvua hizo zimesimama kuharakisha utekelezaji wa miradi.

Amesema NIRC itahakikisha miradi hiyo yote inakamilika kwa wakati na kufikia lengo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Naye Meneja wa Mradi wa Chinangali kutoka NIRC, Mhandisi Saidi Husein Ibrahim, alisema mradi huo uliopo Wilaya ya Chamwino kilomita 45 kutoka Dodoma mjini ukihusisha vijana wa BBT shamba limegawanyika katika katika sehemu nne, ikiwamo sehemu ya hekari 300 ambazo zinatumika na wakulima wa zabibu.

Pia kuna hekari 220 na hekari 400 ambapo kati ya hizo hekari 1150 zinatumika na vijana wa BBT chini ya Wizara ya Kilimo.

Alisema jukumu la tume ni kuhakikisha miundombinu ya umwagiliaji inakamilika chini ya Mkandarasi Mkuu Nakuroi mwenye jukumu la ujenzi wa uzio wenye umeme katika eneo lenye urefu wa km7.8 kuzunguka hekari 1772, ujenzi wa nyumba 46 na nyumba mbili za wataalamu.

Alitaja jukumu lingine la mkandarasi huyo ni kuandaa shamba na kupanda ambalo limefikia zaidi ya asilimia 90.

Mmoja wa vijana ambao ni wanufaika wa mradi wa BBT Chinangali, Yona Remero, amesema maendeleo ya mradi ni mazuri hususani katika uchimbaji wa mabwawa, visima, hadi sasa kuna visima zaidi ya tisa ambavyo vimekamilika.



Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, akipata maelezo jana kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kijiji cha Nyuki Co Ltd, Philemon Kiemi, baada ya kukagua eneo la mto ambao unatumiwa na nyuki kwa ajili ya kunywa maji. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## NEMC, TFS wapanda miti kumuenzi Wangari Maathai

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), wamepanda miti zaidi ya 300 katika msitu asili wa Kazimzumbwi Pugu, kama sehemu ya kumuenzi mwanamazingira nguri Afrika, Wangari Maathai.

Hafla ya kupanda miti hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki kwenye msitu huo ambapo mabalozi wa nchi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao walishiriki pamoja na wanaharakati wa mazingira.

Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Dk. Immaculate Semesi, alisema jamii inapaswa kuhamasishwa umuhimu wa kupanda miti mingi kama sehemu ya kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo wakati mwingine huleta majanga.

Alisema siku hiyo ni muhimu kusherehekea maisha ya Wangari Maathari kwa kuwa alifanyakazi kubwa ya kupanda miti na kuhamasisha utunzaji wa mazingira na kutunukiwa tuzo ya Nobel kwa kazi hiyo.

Mkurugenzi alisema miti ni kiungo muhimu kinachoifanya dunia iendelee kustawi na inasiadia kuchuja hewa safi, kuleta mvua, kusaidia upatikanaji wa chakula na biashara.

"Mama Maathai alikuwa shujaa wa mazingira na mfano bora wa kuigwa kwa Afrika na dunia nzima ikamtambua kwamba yeye ni kinara kwenye utunzaji wa mazingira kwa hiyo tunapaswa kuendelea kumuenzi kwa vitendo kama unavyofanya leo," alisema.

"Sisi NEMC tuna usemi wetu kwamba mazingira ni uhai na moja ya mambo yanayosababisha uhai wa mazingira ni miti kwa hiyo hatuna chaguo lingine zaidi ya kuhakikisha tunapanda miti kwa wingi na kila wakati," alisema.

"Sisi familia nzima ya Afrika lazima tuwe kinara kuhakikisha kwamba mazingira yetu yako safi, yako hai na tunadhibiti hatari yakutokea kwa jangwa, hivyo hali hii ikiendelea hivi ilivyo tunaweza kujikuta tunashindwa kuishi sababu miti ni uhai," alisema Dk. Semesi.

Balozi wa Kenya nchini, Isaac Njenga, alisema kila mtu anapaswa kuona ana deni na jukumu kubwa la kutunza mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Alisema mazingira yanayovuniwa leo ni sababu ya kuwapo kwa watangulizi ambao walijitoa kwa kupanda miti na kuitunza ambao inasiaida kuleta chakula, maji na mahitaji mengine.

## Vituo vya afya Muheza vyapokea vifaa mbalimbali

**Na Steven William, MUHEZA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga imepokea vifaa mbalimbali vya afya katika vituo vinavyotoa huduma za tiba na matunzo (CTC).

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, alisema hayo katika hafla fupi ya makabidhiano ya vifaa hivyo, kwa niaba ya mgeni rasmi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina.

Mombokaleo alisema halmashauri imepokea vifaa hivyo kutoka ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na Shirika la THPS.

Alivitaja vifaa hivyo na idadi yake kwenye mabano kuwa ni majokofu (6), pikipiki (8), centrifuge (9) na printa (8) ambavyo vimegaiwa katika vituo vya kutolea huduma kwa mgawanyiko.

Alisema kuwa huo ni utekelezaji wa Rais Dk. Samia Suluhu katika kuboresha sekta ya afya wilayani humo.

Alimshukuru Rais kwa kutoa vifaa na pikipiki hizo ambazo zitasaidia kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya madaktari hao katika maeneo yao na kuahidi kuwa maelekezo aliyopewa na viongozi wake kutenga fungu la fedha za matengenezo ya pikipiki hizo amelisikia.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, aliwataka watumishi wa sekta ya afya waliokabidhiwa pikipiki kuzitunza na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia shughuli mbalimbali wilayani humo na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Hizi pikipiki ni kwa ajili ya matumizi ya ofisi ikiwamo kwenda maeneo mbalimbali kutatua matatizo ya wananchi na sio vinginevyo...tukikuta umepakia biashara ya viungo vya chai ama kufanyia sherehe za harusi na shughuli nyingine hazihusiani na majukumu yenu ujue kuanzia siku hiyo huna kazi," alisisitiza Mhina.

Alisema kuwa Rais Samia anaipenda Wilaya ya Muheza na ndio maana ameleta fedha za miradi zaidi ya bilioni 2.1 kuboresha sekta ya elimu katika Wilaya ya Muheza anamshukuru sana.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Jamii Afya, Elimu na maji Moses Kisiki alimshukuru Rais kwa kuwawezesha kupata usafiri huo ambao utarahisisha utendaji kazi madaktari katika vituo vyao vya kazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, alishukuru kwa vifaa katika vituo vya kutolea huduma ya afya wilayani humo pamoja na usafiri wa pikipiki kurahisisha utendaji kazi.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuweka utaratibu wa kutenga fedha za matengenezo ya pikipiki hizo ili ziweze kudumu muda mrefu.



Wakimbizi wa ndani Sudan wakipatiwa msaada wa matibabu kutoka kwa madaktari wasio na mipaka. PICHA: REUTER

# Bashe atoa ufafanuzi mchele uliotoka Marekani

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imekanusha uvumi uliosambaa kwenye mitandao ya kijamii kwamba imekubali kupokea msaada wa chakula kutoka Serikali ya Marekani ikisisitiza nchi ina chakula cha kutosha.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo alipokuwa akielezea mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya kilimo.

Alisema ameona kwenye mitandao ya kijamii mjadala mkubwa umeibuka kuhusu Tanzania kupewa msaada wa mchele na maharage uliowekwa virutubisho.

Akifafanua alisema chakula hicho ni mradi unaofanywa na shirika lisilo la kiserikali (NGO) na inafanya shughuli za miradi katika shule za msingi na sekondari.

"Sasa sisi tuliiambia ile NGO kwamba, nchi hii mchele upo na maharage yapo, zile pesa wanazozitumia kuwapa wakulima wa Marekani, wawape wakulima wa Tanzania. Tununue huo mchele na maharage kutoka hapa Tanzania halafu hivyo virutubisho wanavyotaka kuweka, tuweke hapahapa Tanzania wakati sote tunaona," alisema Bashe.

Akizungumzia uvumi unaoenezwa na baadhi ya wanasiasa kuwa serikali imewatekeleza vijana wa mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT), alisema imeibuka mijadala mingi na aliwaambia viongozi wake akiwamo Katibu Mkuu kwamba wasiogope hiyo ni sehemu ya kuboresha utendaji kazi wao.

Alisema kutoka na ukosefu wa ajira nchini, serikali ilikuja na mpango huo na haikutaka kulaumiwa na vijana kwamba waliomaliza chuo hawana ajira na kuondoa maswali yao ya wapi watapata kazi.

Bashe alisema kikwazo kikubwa kwa vijana baada ya kuanza kwa mradi huo kilikuwa ni ukosefu wa ardhi na kwamba kupitia hilo Rais wakati anazindua mradi huo, ardhi iliyokuwapo ilikuwa ni hekari 300 pekee, serikali ikafanya jitihada za kununua hekari zingine laki mbili ambazo mpaka leo zinatumika.

Alisema mpaka sasa vijana 260 wamewapeleka katika Shamba la Chinangali wamejengewa nyumba za kuishi kwa kuwa wamekubali kufanya shughuli za kilimo, na kila mwezi kijana anapewa Sh. 390,000 bure na serikali.

"Nimewaambia wanasiasa msiwatishe watoto wa masikini, kwa sababu wao wanakalia viti vyekundu akitoka tu anapata fedha wale ni watoto wa masikini wanahitaji kuwa na 'future'. Nimewaambia vijana kule kama kuna mtu anataka kuingia kwenye siasa atoke aachane na masuala ya kilimo awaache ambao wapo committed kwenye kilimo," alisisitiza.

Alisema serikali inaendelea kuandaa shamba la hekari 1,700 Chinangali na wamewajengea kiwanda, na Benki ya NMB imetoa Sh. bilioni 12 zitakazotumika kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa mbolea.

### ALAMA ZA SAMIA

Alisema serikali imefanya mradi huo ni mikopo kwa vijana na kwamba kutokana na ugumu kwa mkulima mmoja mmoja kupata mitaji, Rais Samia aliamua kutoa fedha kupitia mfuko wa pembejeo na kuwakopesha kwa riba ya asilimia 4.5 mpaka sasa vijana 118 wamenufaika na serikali imewakopesha jumla ya Sh. milioni 970.

Alisema eneo la tatu la BBT ni 'BBT Extension'. Serikali imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha kilimo sokoine (SUA). Vijana wanaomaliza wanawaingiza kwenye kampuni zinazonunua pamba, wanawaajiri na kuwalipa Sh. 500,000 kila mwezi. Mpaka sasa vijana 250 wameanza.

### BAJETI YA KILIMO KUPAA

Bashe alisema Wakati Rais anaingia madarakani, eneo la umwagiliaji katika nchi lilikuwa hekta 726,000. Mwaka wa kwanza Rais alitoa fedha bajeti ya umwagiliaji zisizozidi Sh. bilioni 50 mpaka Sh. bilioni 361.

Kikubwa alichokifanya ni kuwekeza kwa kiwango kikubwa cha fedha ya umma kwenye kuendesha shughuli za uzalishaji.

Aliongeza bajeti kutoka Sh. Bil 290 hadi kufikia Sh. Bil. 750, na kwamba kwa mwaka huu bajeti ikafika hadi Sh. Bil. 970 na matarajio yao kwa mwaka ujao bajeti ya sekta ya kilimo ifikie Sh. Trilioni 1.

"Leo anafanya upembuzi yakinifu wa mabonde yote tuliyonayo ya nchi hii. Inawezekana asiyakamilishe yeye, atakuja kuyakamilisha mtu. Na hiyo ndio vision ya muda mrefu. Rais ameamua kuchukua 'approach' sahihi kwenye kilimo.

Alisema nchi itaandika historia kwa mara ya kwanza kufanya mradi wa kwanza wa kutumia maji kutoka Ziwa Victoria baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu. "Tunahahangaika ukame, kila siku mvua zikinyesha kuanzia Morogoro Dodoma hatupiti kuna maeneo tunaita yana ukame. Kwa mara ya kwanza mwaka huu serikali ya Awamu ya Sita imeanza ujenzi wa mabwawa 100 kuvuna maji ya mvua yanayomwagika barabarani.

"Pia tuna mradi wa kukusanya maji yanayojaa barabarani kwa ajili ya kupambana na ukame na kukuza kilimo cha umwagiliaji miradi hii imeshatangazwa na makandarasi wapo site.

Alisema lengo la serikali ndani ya miaka saba ijayo ni kuchimba visima 67,000 kwa ajili ya wakulima wadogo ambapo visima hivyo jumla vitatupatia ekari milioni 2.5 ambazo zitakuwa zinamwagiliwa lengo ikiwa ni kumfanya mkulima abaki shambani.

Kadhalika, ndani ya miaka mitatu ya serikali imefufua kampuni iliyoanzishwa na Baba wa Taifa ya Tanzania Fertilizer Company kwa kuipatia mtaji mwaka wa kwanza wastani wa Shilingi bilioni sita, mwaka wa pili ikapatiwa Sh. bilioni 40 na sasa mtaji umefika Sh. bilioni 116. Kampuni hiyo sasa, imekuwa moja ya kumi bora katika usambazaji wa mbolea nchini.

"Mwaka jana tumepata shida ya bei korosho kwenye Soko la Dunia na tumeauza kwa bei ya chini. Njia pekee hapa ya kumsaidia mkulima ni kuongeza thamani ya zao hili.

"Kwenye hili serikali imeanzisha mradi unaitwa 'MARANJE' na mpaka sasa tunatumia wastani wa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kujenga Maranje maghala yatakayosubiri mwekezaji alete mashine kwa ajili ya kubangua Korosho na malengo yetu ifikapo 2026/27 Korosho yote ibanguliwe nchini," alisema.

# Niger yavunja mkataba wa kijeshi na Marekani

**NIAMEY, Niger**

MSEMAJI wa utawala wa kijeshi nchini Niger, Kanali Amadou Abdramane, amesema utawala huo umebatilisha mkataba wa kijeshi ambao uliruhusu kuwapo kwa wanajeshi na wafanyakazi wa kiraia kutoka Wizara ya Ulinzi ya Marekani katika ardhi ya taifa hilo.

Ilielezwa kuwa uamuzi huo utakaoanza mara moja, umekuja baada ya ziara ya maofisa wa Marekani wakiongozwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje kwa Masuala ya Afrika, Molly Phee pamoja na Jenerali Michael Langle kamanda wa Kamandi ya Marekani Afrika.

Abdramane, akizungumza kwenye televisheni ya taifa hilo jana, alisema ujumbe wa Marekani haukufuata taratibu za kidiplomasia na kwamba Niger haikujulishwa kuhusu waliomo ndani ya ujumbe wala tarehe ya kuwasili kwao au ajenda yao.

Pia alisema majadiliano yao yalihusu mpito wa sasa wa kijeshi nchini Niger, ushirikiano kati ya nchi hizo mbili na maamuzi ya Niger ya kushirika katika mapambano dhidi ya wanamgambo wenye uhusiano na al-Qaida na kundi la Islamic State.

Ilielezwa kuwa tangu mapinduzi yalipofanyika Julai, 2023, utawala wa kijeshi wa Niger, kama walivyo watawala wa kijeshi katika nchi jirani za Mali na Burkina Faso, wameifukuza Ufaransa na majeshi mengine ya Ulaya na kuigeukia Russia kwa msaada.

"Niger inasikitika kuwa azma ya ujumbe wa Marekani ni kuwanyima watu wa Niger haki ya kuchagua washirika wao na aina ya ushirika wenye uwezo wa kweli wa kusaidia katika mapambano dhidi ya ugaidi.

"Pia serikali ya Niger inalaani vikali kwa nguvu tabia ya kujishusha chini inayoambatana na vitisho vya kulipiza kisasi kutoka kwa ujumbe wa Marekani kwa serikali ya Niger na watu," alisema.

Aidha, ilielezwa kuwa kuna kiasi cha wanajeshi 1,100 wa Marekani nchini Niger hadi mwaka jana, ambako Marekani inafanya shughuli za kijeshi kutoka kwenye kambi mbili ikiwemo ya ndege zisizo na rubani inayojulikana kama Air Base 201, iliyojengwa karibu na Agadez katikati mwa Niger iliyogharimu zaidi ya dola milioni 100.

Ilielezwa kuwa tangu mwaka 2018 kambi hiyo imetumiwa kuwalenga wanamgambo wa Islamic State na Jama'at Nusrat al-Islam wal Muslimeen (JNMI) na mshirika wa al-Qaida, katika eneo la Sahel.

Abdramane alisema hadhi na uwepo wa wanajeshi wa Marekani nchini Niger ni kinyume cha sheria na imekiuka kanuni za kikatiba na demokrasia kwasababu, kwa mujibu wa msemaji, iliamuliwa na upande mmoja kwa taifa hilo la Afrika mwaka 2012.

Alisema Niger haikuwa na habari kuhusu idadi ya raia na wanajeshi wa Marekani walio katika ardhi au vifaa vimepelekwa huko na kwa mujibu wa mkataba, jeshi la Marekani halina jukumu la kujibu ombi lolote kwa msaada dhidi ya wanamgambo.

"Kutokana na yote hayo, serikali ya Niger, tunabatilisha haraka sana mkataba unaohusiana na hadhi ya wanajeshi wa Marekani pamoja na wafanyakazi wa kiraia katika Wizara ya Ulinzi ya Marekani kwenye eneo la Jamhuri ya Niger," Abdramane alisema.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilitafutwa ili kutoa maoni juu ya suala hilo bila mafanikio.

**VOA**

# JULIO AFICHUA KILICHOKUWA KIKIITAFUNA SINGIDA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuanza kazi na ushindi, Kocha Mkuu mpya wa Singida Fountain Gate, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema kilichokuwa kinaiathiri timu hiyo kiasi cha kushindwa kupata ushindi kwenye mechi nane mfululizo ni wachezaji wake kutokuwa na utimamu wa mwili.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Namungo, Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na timu yake kushinda bao 1-0, Julio alisema baada ya kuingia tu kwenye timu hiyo, kitu alichobaini ni ukosefu wa fiziki kwa wachezaji ndiyo ulikuwa ukiwatafuna.

"Nimegundua timu hii ilikuwa na matatizo kadhaa, kikubwa hawako vizuri kwenye utimamu wa mwili, lakini kutokana na maelekezo niliyowapa wameweza kutekeleza na kupata ushindi.

"Leo tumeshinda, kilichobaki sasa ni kuwaandaa vizuri kwa sababu nitakuwa nao kwa mwezi mzima kwenye mazoezi wakati ligi imesimama, nafikiri ile Singida ya mwanzo itarudi sasa hivi," alisema Julio, akiiongoza timu hiyo kushinda kwa mara ya kwanza baada ya mechi tisa.

Awali timu hiyo ilicheza mechi nane bila kupata ushindi, ambapo mara ya mwisho kushinda ilikuwa ni Novemba 27, mwaka jana, ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1 nyumbani, na baada ya hapo ikicheza mechi nane, ikipoteza tano na sare tatu.

Ilianza kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, na sare nyingine na mechi inayofuata ikatoka suluhu dhidi ya KMC, kabla ya kwenda kukutana na kipigo cha bao 1-0, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, dhidi ya Geita Gold.

Ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, kabla ya kupata kipigo kingine cha mabao 3-1 dhidi ya Prisons na kwenda kutoa sare ya bao 1-1, dhidi ya Taboara United.

Baada ya hapo ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Azam kabla ya kubamizwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kocha Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera, kwa upande wake alilalamikia maamuzi, akidai wamelazimishwa kufungwa.

"Tumelazimishwa kufungwa, timu yangu imecheza vizuri sana kama kungekuwa na uchezeshaji mzuri wala tusingefungwa, hata kama tusingeshinda, lakini tusingepoteza," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Anna Gidarya (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa maandalizi ya Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Utalii maarufu 'Lake Zone Cultural and Tourism Festival', linaloandaliwa na Kilimanjaro One Travel and Tours. Wengine kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Christina Emmanuel, Mkurugenzi Mohamed Hatibu, Ofisa Maendeleo ya Vijana, Zena Mchujuko, Ofisa wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Gabriel Awe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tamasha la Utamaduni na Utalii lazinduliwa Simiyu

**Na Jumanne Juma**

MAANDALIZI ya tamasha kubwa la Kimataifa la Utamaduni na Utalii linalojulikana kama Lake Zone Cultural and Tourism Festival, linalotarajiwa kufanyika Julai mwaka huu, yameanza baada ya kuzinduliwa rasmi Bariadi mkoani Simiyu juzi.

Uzinduzi huo ulifanywa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, aliyewakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Anna Gidarya, na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, wadau wa utamaduni na utalii kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na jirani.

Katika uzinduzi huo, mkuu huyo wa mkoa aliipongeza Kampuni ya Kilimanjaro One Travel and Tours kwa kubuni tamasha hilo la Utamaduni na Utalii kwa Kanda ya Ziwa na kuamua lifanyike katika Mkoa wa Simiyu.

Alisema utamaduni ni jambo kubwa la kujivunia na ni lazima uenziwe na kuendelezwa kwa nguvu zote kwa sababu ni urithi tuliopokea kutoka kwa babu zetu, hivyo na sisi hatuna budi kuuendeleza.

Aidha, alisema tamasha hili litasaidia sana kutangaza utamaduni wa Mkoa wa Simiyu kupitia shughuli mbalimbali zitakazofanyika na hivyo kuufanya ufahamike zaidi ndani na nje ya nchi.

"Nimearifiwa kuwa leo ni uzinduzi tu ili tupate kionjo cha kinachotarajiwa kufanyika mwezi wa saba mwaka huu, ambapo kutakuwa na tamasha kubwa la siku tatu mfululizo na litahusisha watu zaidi ya 7,000 wakiwamo washiriki wa maonyesho.

"Hii ni hatua kubwa na ni fursa kwa washiriki kufanya biashara na kujifunza mambo mbalimbali wakati wa tamasha, hivyo, sekta ya utalii na utamaduni itakuwa kwa sababu wageni wote watakaokuja watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya mkoa wetu na kujionea vivutio mbalimbali vikiwamo vya utamaduni," alisema.

Alitoa wito wa maandalizi ya tamasha hilo kubwa kufanyika mapema ili kupata washiriki wengi kutoka ndani na nje ya nchi huku pia akiwapongeza waandaaji kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita za kuhakikisha utamaduni unatangazwa na kuufanya kivutio kikubwa cha watalii wa ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na waandaaji wa tamasha hilo kuhakikisha linafanyika kila mwaka na kuwa chachu ya maendeleo kiutamaduni na kiuchumi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimanjaro One Travel and Tours, Christina Emmanuel, alisema kuwa hii ni mara ya kwanza kwa kampuni hiyo ambayo inajihusisha na masuala ya utalii na utamaduni kuandaa tamasha hilo ambalo wanaamini litakuwa na mwitikio mkubwa kwa wakazi wa Simiyu na mikoa ya jirani.

"Tamasha hili linatarajiwa kufanyika mwezi wa saba na ninayo furaha kukufahamisha kuwa litafanyika kwa siku tatu mfululizo Julai 5, 6 na kilele chake kitakua Julai 7, mwaka huu ambapo pamoja na mambo mengine tunategemea kuwa na maonyesho mbalimbali ya masuala ya utamaduni na utalii katika Uwanja wa Halmashauri na kuwavutia washiriki na watazamaji zaidi ya 7000 kwa siku hizi tatu. Pia litakuwa na vionjo mbalimbali ikiwamo ngoma inayohusisha makabila ya Wagika na Wagulu," alisema.

Naye Ofisa wa Baraza la Sanaa nchini (BASATA), Gabriel Awe, amewasifu waandaaji kwa kuandaa tamasha hilo katika kuendeleza utamaduni na utalii hapa nchini, akitoa wito kwa wadau wengine kuliunga mkono kwa hali na mali.

"Ni tamasha kubwa la aina yake ambalo sisi kama Watanzania tunapaswa kujivunia kuwa hili ni la kwetu kwa maendeleo ya utamaduni na utalii wetu."

## Manula aja na Air Manula Sports

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya michezo unakuwa rahisi zaidi nchini, mlinda mlango namba moja wa Klabu ya Simba, Aishi Manula, ameamua kuzindua duka litakalokwamua changamoto hizo.

Aliyasema hayo jana wakati alipokuwa anazindua duka lake la vifaa vya michezo alililopa jina la 'Air Manula Sports', lililopo Morocco, Dar es Salaam.

"Wapo wanamichezo wengi wenye uwezo wa kufungua maduka, ila wachache ndio wenye vifaa vyenye ubora wa juu, nimeamua kufungua duka hili kwani mara nyingi tumekuwa tukiuziwa viatu ambavyo havina ubora," alisema Manula.

Alisema duka hilo litawarahisishia wanamichezo kupata vifaa bora na kudai hayo ni mafanikio aliyoyapata kutokana na kazi yake ya soka.

Mlinda mlango huyo aliwataka wachezaji wenzake kutumia fursa vizuri kipindi ambacho bado wanacheza mpira ili baada ya kustaafu wawe na vitega uchumi vitakavyowasaidia kupata kipato, kuliko kutegemea kazi moja.

"Ninawashauri wanamichezo wenzangu kutumia fursa wakati bado tunacheza mpira ili hata tukiuacha tuendeleze miradi mingine," alisema mlinda mlango huyo.

## Tanesco kileleni Ligi Daraja la Pili

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Tanesco FC, imekwea juu ya msimamo wa Ligi Daraja la Pili, maarufu kama 'First League', kwenye Kundi B, baada ya juzi kuiadhibu Mapinduzi mabao 4-0, mechi iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Wakati Tanesco ikiongoza Kundi D, Nyumbu inaongoza kwenye Kundi A licha ya kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya African Sports.

Ushindi huo mnono wa Tanesco, unaifanya timu hiyo kuongoza kundi hilo kwa mara ya kwanza, ikiwa na pointi 23, sawa na Mapinduzi iliyokuwa ikiongoza kwa muda mrefu, lakini ikiwa na mabao mengi ya kufunga.

TRA, ambayo hivi karibuni ilibanjuliwa mabao 6-0 na Simba, Kombe la FA, inashika nafasi ya tatu na pointi zake 21, Rhino Rangers ya nne, pointi zake ni 20, wakati Mwadui FC inashika nafasi ya tano, ina pointi 16.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE HAITAKI ARSENAL

MSHAMBULIAJI nyota wa Klabu ya Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, amesema kamwe hatojiunga na Arsenal mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

### PALMER NYONGEZA MSHAHARA

WINGA Cole Palmer mwenye umri wa miaka 21, anayecheza katika Klabu ya Chelsea, anatarajiwa kupokea nyongeza kubwa ya mshahara. Nyongeza hiyo inakuja ikiwa bado hata hajatimiza mwaka mmoja tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea Manchester City. ***(Star)***

### TODIBO KUKWAMISHWA

VIONGOZI wa Klabu ya Nice wanajiandaa kukwamisha jitihada za Manchester United kutaka kumsajili beki wao wa kati Mfaransa Jean-Clair Todibo, 24. ***(Football Insider)***

### WERNER MUDA WA MWISHO

KLABU ya RB Leipzig ya Ujerumani imeipatia Tottenham Hotspur muda wa mwisho wa kumnunua mshambuliaji Timo Werner mwenye umri wa miaka 28, ambaye walimsajili kwa mkopo tangu Januari. ***(Express)***

### ENDERSON MKATABA MPYA

KLABU ya Manchester City inataka kuanzisha mazungumzo ya mkataba mpya na golikipa wao, Ederson, 30. ***(Star)***

### RAPHINHA ATAKIWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Raphinha mwenye umri wa miaka 27, ni moja kati ya wachezaji vinara wanotaka kusajiliwa katika Ligi Kuu ya Saudi Arabia mwishoni mwa msimu. ***(Sport)***

### RODRIGO NAYE AWINDWA

KLABU ya Al-Ahli ya nchini Saudi Arabia imeweka wazi nia yao ya kumsajili kiungo wa Argentina, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 29, kutoka Klabu ya Atletico Madrid. ***(Fichajes)***

### NEWCASTLE, CHELSEA VITANI

KLABU ya Newcastle United na Chelsea zinajiandaa na vita vya kutaka kumsajili winga raia wa Ufaransa anayeichezea Klabu ya Lyon, Rayan Cherki, 20. ***(Fichajes)***

### MIN-JAE HANA FURAHA

MLINZI wa Klabu ya Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae mwenye umri wa miaka 27, hana furaha na maisha katika klabu hiyo ya Ujerumani. Kim alishawahi kuwindwa na Manchester United. ***(t-online, via Football Transfers)***

### AMRABAT BASI TENA

KLABU ya Manchester United haitarajii kumsajili moja kwa moja Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27, mwishoni mwa msimu huu. Amrabat yupo United kwa mkopo akitokea Fiorentina, tayari Klabu ya Juventus ina nia ya kumsajili raia huyo wa Morocco. ***(Gazzetta dello Sport)***

### WIEFFER AWINDWA BARCA

BARCELONA inatarajiwa kujaribu tena kumsajili kiungo wa Klabu ya Feyenoord, Mholanzi Mats Wieffer, 24. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE AANDIKA REKODI MPYA LIGI BUNDESLIGA

Ni ya mabao mengi kuwahi kuwekwa na mchezaji yeyote msimu wake wa kwanza katika...

**MUNICH, Ujerumani**

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Harry Kane, alifunga bao lake la 31 la ligi, lililovunja rekodi, huku Jamal Musiala akiongeza mengine mawili katika ushindi wa 5-2 dhidi ya wenyeji, Darmstadt 98 Jumamosi na kuwafanya mabingwa hao wa muda wote kufikisha pointi saba nyuma ya vinara Bayer Leverkusen kwenye Bundesliga.

Kane aliiweka mbele Bayern 2-1 ambayo itamenyana na Arsenal katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi ujao, na kufikisha jumla ya mabao 31 kwenye ligi, zaidi ya mchezaji yeyote kufunga katika msimu wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Pia ni ligi binafsi bora kwa nahodha huyo wa England ambaye ndio usajili ghali zaidi kwa Bundesliga baada ya kutua huko kwa euro milioni 100.

Lakini alitolewa nje akiwa amejeruhiwa katika dakika ya 81 baada ya kuteleza na kujikunja kifundo cha mguu. "Alijikwaa na kuanguka kwenye wavu na kukunja kifundo cha mguu," alisema kocha wa Bayern Thomas Tuchel.

"Bado hatujajua ameumia kiasi gani. Inabidi tusubiri na kuona."

England, ikijiandaa kwa Euro 2024 nchini Ujerumani Juni, itacheza na Brazil Machi 23 na Ubelgiji siku tatu baadaye.

"Kwa ujumla tuna furaha kwa ushindi unaostahili. Tuliendelea kutengeneza nafasi na tulistahili mabao tuliyofunga," alisema Tuchel.

"Imekuwa wiki nzuri na tuna mazingira mazuri sana na tunafanya mazoezi vizuri. Tuna furaha kuendelea na mbio zetu baada ya ushindi wetu dhidi ya Lazio (kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya) na Mainz wiki iliyopita," alisema kocha huyo ambaye ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Ushindi huo unaifanya Bayern kufikisha pointi 60 katika nafasi ya pili, pointi saba nyuma ya Leverkusen ambao jana Jumapili walicheza na Freiburg.

HABARI MICHEZO

# SON ALIA NA WACHEZAJI SPURS

**LONDON, England**

NAHODHA wa Tottenham Hotspur, Son Heung-Min, amesema wachezaji wanahitaji "kujitazama kwenye kioo" baada ya kipigo "kisichokubalika" cha 3-0 Jumamosi kutoka kwa Fulham kutilia shaka kumaliza katika nne bora kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Ushindi huo ungewaweka mbele ya Aston Villa kwenye nafasi ya kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Spurs walionesha mchezo hafifu na kushindwa kufunga katika mechi ya ligi kwa mara ya kwanza msimu huu. "Inasikitisha sana na inakatisha tamaa. Kila mtu anapaswa kujitazama kwenye kioo na kusema 'ni kosa langu'," Son alisema.

"Haikuwa nzuri vya kutosha. Hatukuweka bidii ambayo tumeweka msimu huu. Uchezaji, mtazamo haukuwa mzuri vya kutosha. Kila mtu anahitaji simu kubwa ya kuamka."

Kiwango hicho kilishangaza zaidi ikizingatiwa ushindi wa Tottenham wa mabao 4-0 dhidi ya Villa wikendi iliyopita. Son Heung-Min alikosa nafasi nzuri ya kuwaweka Tottenham mbele katika kipindi cha kwanza.

"Kwenye Ligi Kuu ikiwa wewe hauko tayari kujitoa kwa asilimia 100, utapata adhabu," alisema fowadi huyo wa Korea Kusini.

"Aston Villa ni timu ya ajabu, lakini pia Fulham. Hii ni hatua mbili nyuma, sasa tunatakiwa kupiga hatua mbele, haikubaliki, nikiwamo mimi ilikuwa haikubaliki.

"Tunawakilisha timu za Ligi Kuu, tunawakilisha Tottenham. Hii haikuwa karibu na kile ambacho tumekuwa tukifanya msimu huu. Inasikitisha sana kutazama hili. Mashabiki hawastahili hili. Kupoteza hii ilikuwa ngumu sana."

Kocha wa Spurs, Ange Postecoglou alisema alisikitishwa sana na matokeo ya timu yake kipindi cha pili.



## Real Madrid sasa yambania Mbappe

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imeliarifu Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), kwamba hawatatoa mchezaji yeyote kwa ajili ya Michezo ya Olimpiki ya msimu huu wa majira ya joto, na hivyo kutoa pigo kubwa kwa Kylian Mbappe ambaye anataka kucheza kwenye mashindano hayo.

Mbappe amethibitisha uamuzi wake wa kuondoka Paris Saint-Germain na ameripotiwa kukubaliana na Madrid. Wakati wa mazungumzo Real Madrid, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, aliweka wazi kuwa anataka kupewa nafasi ya kuiwakilisha Ufaransa kwenye michuano ya Olimpiki ya majira ya joto kule Paris.

Hatua kama hiyo ingemfanya Mbappe kukosa mechi za maandalizi ya msimu mpya na wiki za mapema za kampeni ijayo.

Kwa vile Olimpiki si mashindano yanayotambuliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (Fifa), klabu hazina wajibu wa kuwaachia wachezaji wao na Madrid haitaruhusu mchezaji wao yeyote kushiriki michuano hiyo.


Madrid wamewasiliana na FFF kuwafahamisha kwamba wachezaji wao wote wa Ufaransa - Ferland Mendy, Eduardo Camavinga na Aurelien Tchouameni – watazuiwa kwenye mashindano hayo msimu huu wa joto, na bila shaka hilo litatumika kwa Mbappe ikiwa atajiunga na klabu hiyo.

Timu ya Olimpiki itaongozwa na Thierry Henry, ambaye alikiri changamoto katika kushawishi klabu kuwaachia nyota wao wakuu.

"Sio suala la kukata tamaa kwa sababu ninaweza kuelewa kila kitu," alisema. "Lazima tuelewe jambo moja, uamuzi unatoka kwa klabu.

"Timu zinahitaji wachezaji wao mwanzoni mwa msimu, timu za nje hazifikirii Olimpiki au sisi, lakini juu yao, iko mikononi mwa klabu. Tunajaribu kujadili na kuona nini kinaweza kutokea, lakini ikiwa klabu itashikilia uamuzi wake, ni vigumu kwetu kufanya kitu."

Kocha mkuu wa Ufaransa Didier Deschamps aliongeza: "Sio mimi ninayeamua timu. Thierry akiamua kuchukua mchezaji na klabu ikakubali, atakuwa kwenye timu."




## Ivan Toney aitaja klabu atakayojiunga nayo

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Ivan Toney, amefichua kwamba uhamisho wake bora utakuwa kwa mabingwa mara 14 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid.

Toney anatamani kuingia kwa nguvu katika mipango ya kocha Gareth Southgate kwenye euro 2024 na aliitwa Alhamisi kwenye kikosi cha wachezaji 25 cha England kwa ajili ya mechi zijazo za kimataifa za Machi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alikosa miezi sita ya kwanza ya msimu wa 2023/24 baada ya kufungiwa miezi nane na FA kwa kukiuka kanuni za kamari, lakini anatazamwa kama mmoja wa washambuliaji wa kati bora zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Mabao manne katika mechi tisa baada ya kurudi dimbani yamevutia umakini wa Kocha wa England, Southgate, ingawa mustakabali wa muda mrefu wa Toney umetawala vichwa vya habari katika miezi michache iliyopita.

90min ilifichua Novemba kwamba wawakilishi wa Toney walikuwa wamekutana na Arsenal na Chelsea juu ya uwezekano wa kujiunga nao, wakati wapinzani wa London Tottenham Hotspur pia wanajulikana kumtaka baada ya kuondoka kwa Harry Kane msimu uliopita wa majira ya joto.

Mwaka jana, alifichua kuwa atakuwa tayari kujiunga na Arsenal au klabu yake ya utotoni, Liverpool.

Lakini akizungumza na Sky Sports, Toney alichanganya klabu tofauti alipoulizwa kuhusu majira yake bora ya jota yatakuwaje.

"Ikiwa Brentford wataniuza watapata fedha zao, nitahamia Madrid na ni sawa," alisema Toney.



HABARI MICHEZO

# AZAM YATATHMINI OFA ZA SIMBA, AL HILAL KWA DUBE

Na Adam Fungamwango

MKUU wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano, Azam FC, Thabit Zakaria maarufu Zaka Zakazi, amesema kwa sasa wapo katika hatua ya kuzifanyia tathmini ofa za Klabu ya Simba na Al Hilal ya Sudan zilizotolewa kwa ajili ya kumtaka straika wao, Prince Dube.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Zaka Zakazi, alisema bado wanaruhusu ofa kutoka kwenye klabu zingine zinazohitaji huduma yake, huku akishangaa jambo hilo kuwa na mihemko zaidi kuliko utaratibu uliowekwa.

Hivi karibuni klabu hiyo ilitoa taarifa ya kupata ofa kutoka Simba na Al Hilal, zikimhitaji mchezaji huyo ambaye kabla ya hapo alikuwa ameshaandika barua ya kuvunja mkataba na klabu hiyo.

„Ni kweli ameomba kuvunja mkataba na sisi tumemkubalia, lakini kisheria kuna vitu anatakiwa afanye ili kuuvunja, pamoja na hayo haituzuii sisi tusipokee ofa kutoka klabu zingine kwa sababu bado ni mchezaji wetu mpaka pale atakapotekeleza vipengele vya kuuvunja.

„Nimeona kuna baadhi ya wachambuzi na mashabiki wanahoji eti mtu anataka kuvunja mkataba awe huru achague timu anayoitaka yeye, halafu tunapokea ofa, sisi hatutomlazimisha, tumepokea ofa, sasa zinafanyiwa tathmini, zikikubalika tunamwita mwenyewe na kumwambia, au tutaiambia klabu iliyoteuliwa kuongea naye, wala hatutomlazimisha," alisema Zakazi.

Alisema tathmini inayofanywa siyo ya pesa peke yake, bali kuna vitu mbalimbali, kama vile klabu anayokwenda kama ikimuuza Azam itapata nini na vitu vingine vingi ambavyo kama klabu inayomtaka ikikubali, basi kitakachofuata ni kumjulisha mchezaji mwenyewe.

„Suala hili lipo duniani kote, lakini nashangaa hili la Dube limekuwa kama na mihemko, wengine wanatulaumu kwa nini tumetangaza, sisi kwetu siyo siri, tumeweka wazi, hakuna udhalilishaji wala kanuni iliyovunjwa," alisema.




## Chama: AL Ahly wetu, Job atoa siri Yanga

INATOKA UK. 24

kutikiswa, unapokuwa kwenye timu kubwa kama hizi, kabla ya sisi kufunga hatutakiwi kuruhusu bao ili tuwe na faida na uwezekano mkubwa wa kupata ushindi, kama tutaruhusu ina maana tunakuwa tumejitia wenyewe kwenye hali ngumu, kwa hiyo sisi mabeki tunapotoka kambini kwenda uwanjani, jukumu letu namba moja ni kukaba wapinzani wasilete madhara siyo kwa asilimia mia moja, hapana ni mia mbili," alisema Job.

Alisema timu yoyote ambayo hairuhusu mabao kizembe, ina asilimia kubwa ya kupata ushindi kwa sababu ikipata bao moja tu linaweza kabisa kuipa pointi tatu, na hivyo ndivyo kikosi chao kilivyo hivi sasa.

Yanga imeruhusu mabao tisa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ikiwa ni idadi ndogo ya mabao kuliko timu yoyote ile katika ligi hiyo.

Job alisema pamoja na wao kama mabeki kupanga mikakati, lakini kipa wao Diarra amekuwa mhimili mkubwa kwa yote hayo.

Alisema Diarra ni kipa mzuri sana, lakini uzuri wake pia unaongezeka kutokana na kuongea muda wote na mabeki huku akiwafokea.

"Djigui ni mkali sana, hasa tunapokuwa tunafanya makosa ya kizembe, ni mtu mmoja ambaye anafoka sana, lakini mimi namwelewa kwa sababu hii ni kazi na kila mtu hataki kufanya vibaya kwenye nafasi yake, vile anavyofoka inatupa sisi nguvu ya kupambana ili kutoruhusu bao rahisi," alisema.

Kuhusu lugha ya maelewano alisema katika soka wachezaji wanapokaa kambini wanatengeneza lugha moja inayoweza kuwafanya wawe na mawasiliano mazuri uwanjani.

"Siku hizi kidogo anajua maneno machache, sogea, kushoto, kulia, zamani alikuwa hajui Kiswahili kabisa, Diarra hajui Kingereza, anaongea Kifaransa, lakini sisi wachezaji tuna lugha zetu na tunaelewana, halafu anaongea hata lugha ya kwao, sisi tunamwelewa, na hii yote tunaelekezana tukiwa kambini, tunamfundisha lugha yetu, na yeye anatupa lugha ya kwao, maana yake, mambo yanakwenda," alifichua beki huyo.

## Stars 23 wapaa kuivaa Bulgaria

INATOKA UK. 24

CF - Hispania).
Viungo ni Feisal Salum na Yahya Zaydi (Azam FC), Mudathir Yahya (Yanga), Morice Michael (RFK Novi Sad - Serbia), Himid Mao(Telaea El Gaish SC - Misr) na Tarryn Allarakhia (Wealdstone - Uingereza)
Washambuliaji ni Clement Mzize (Yanga), Simon Msuva (Alnajmah FC - Saudi Arabia), Kibu Denis (Simba), Abdul Suleiman (Azam FC), Ben Starkie (Ilstone Town - Uingereza) na Charles M'mombwa (Macarthur - Australia).

# CAF kutoa darasa la leseni za klabu Z'bar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeandaa mafunzo maalum ya leseni za klabu (club license), yatakayofanyika leo na kesho visiwani hapa.

Katibu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai, akizungumza na mwandishi wa habari hizo ofisini kwake Mbuyu Mnene jana, alisema washiriki ni viongozi wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar pamoja na watendaji kutoka shirikisho hilo.

Alisema mafunzo hayo ambayo hufanyika kwa kila nchi mwanachama wa CAF, yatafanyika katika Beitras nje kidogo ya mji wa Zanzibar na yatahusu kujifunza kuhusu ujazaji wa taarifa za klabu kwa njia ya mtandao.

"Kama tunavyojua klabu hizi kuna vitu vinatakiwa wawe navyo ili kuweza kupata leseni ikiwamo kuwa na timu za vijana, wanawake, kuwa na utaratibu wa kitaasisi na vitu vingine vingi ambavyo vimeelekezwa ili kuwa sahihi na kisasa katika uendeshaji uliosahihi," alisema Vuai.

Hata hivyo, alisema mafunzo hayo yatakuwa ni namna ya kuweza kutumia na kuendesha klabu katika mfumo wa kidigitali.

Alisema mafunzo hayo yanatakiwa kutolewa kwa nchi zote wanachama wa CAF na kwamba Zanzibar pia imetakiwa kuyafanya ili kuweza kutekeleza matakwa ya leseni za klabu.

Alisema mpaka sasa mafunzo hayo yameshafanyika Tanzania Bara, Uganda na sasa hivi wanamalizia Rwanda na kisha Tanzania Visiwani (Zanzibar), ambapo wakufunzi watatoka CAF.

Kuhusu kuwashirikisha watendaji wao, alisema wamefanya hivyo ili kuwaandaa mapema hasa kwa kuwa Zanzibar inatarajiwa kuandaa mashindano makubwa ya kimataifa ndani ya mwaka huu.

Alisema kutokana na hali hiyo wameona ni vema wakawafunza hasa kwa kuwa wao watakuwa ni wasimamizi wakubwa katika mashindano hayo ambayo yanafuata kanuni zote za FIFA na CAF.

Alisema awali walipanga kushirikisha na viongozi wa klabu za Kanda, lakini kwa mujibu wa kanuni bingwa wa Ligi Kuu ndiye anayeshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na wa Kombe la FA, atashiriki Kombe la Shirikisho, ingawa pia inawezekana akatoka katika klabu za Kanda.

"Lakini katika hali ya kawaida na ukubwa wa ushiriki wa mashindano, tumeweza kukamilisha yale matakwa ya kikanuni, lakini kwa mwaka huu tutashirikisha klabu hizo za Ligi Kuu na mwakani tutajipanga kushirikisha na za Kanda," alisema.


# Michezo

Jumatatu Machi 18, 2024

Nipashe


**Kane aandika rekodi mpya Ligi Bundesliga** UKURASA 21





Chama

Job

# CHAMA: AL AHLY WETU, JOB ATOA SIRI YANGA

●●●Ni mkakati wa ushindi robo fainali CAF, huku Diarra naye akitajwa kuwa sababu ya...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kiungo wa Simba, Clatous Chama, akikiri kuwa mechi yao dhidi ya Al Ahly katika hatua ya robo fainali, itakuwa ngumu, lakini sasa ni muda wao wa kuandikia historia katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, beki wa Yanga, Dickson Job amefunguka na kufichua siri ya ushindi wa mechi zao, pamoja kwa kuwa timu iliyoruhusu mabao machache kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Simba inatarajiwa kuanzia nyumbani katika mchezo wa robo fainali ya michuano hiyo dhidi ya Al Ahly ya Misri unaotarajiwa kuchezwa Machi 29, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam huku kesho yake Yanga ikiikaribisha Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini uwanjani hapo.

Akizungumza na Nipashe jana, Chama alisema itakuwa mechi ngumu kwa kuwa wanafahamu ubora wa Al Ahly, hivyo watacheza kwa kuwaheshimu kwa sababu wanahitaji kufanya vizuri ili kuandika historia mwaka huu.

Alisema malengo yao makubwa ni kupambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo ujao dhidi ya Al Ahly kupata matokeo nyumbani, jambo ambalo anaamini benchi la ufundi litafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika michezo iliyopita.

“Malengo yetu ni kuona tunavuka robo fainali baada ya misimu minne kuishia hatua hii, Al Ahly si wageni kwetu, tumekutana nao mara nyingi, ni timu nzuri na bora lakini hatuwaogopi tunawaheshimu na tuko tayari kupambana,” alisema kiungo huyo aliyeenda kwao Zambia kwa ajili ya majukumu ya timu ya taifa.

Wakati Chama akieleza hayo, beki wa Yanga, Job amefunguka na kufichua siri ya ushindi wa mechi zao, pamoja kwa kuwa timu iliyoruhusu mabao machache kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, alisema mpango mkakati wao namba moja ni kutoruhusu bao lolote kizembe kwenye mechi yoyote, na hiyo huwapa nafasi kubwa ya kushinda mechi, akimtaja kipa wao, Djigui Diarra, kuwa ndiye kiongozi wa mpango huo, na si kwa sababu ya umahiri wake tu wa kudaka, lakini ukali alionao kwa mabeki.

“Asilimia 60 au 70 za ushindi wa timu yetu unatokana na kutoruhusu wavu

INAENDELEA UK. 23

# Stars 23 wapaa kuivaa Bulgaria

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Taifa Stars kimeondoka leo saa 12:00 asubuhi kuelekea nchini Azerbaijan kwa ajili ya michezo ya kirafiki ya FIFA Series 2024, ambapo kikiwa huko kitacheza mechi mbili.

Stars inatarajia kucheza mechi hizo Ijumaa wiki hii na Jumatatu ijayo dhidi ya Bulgaria na Mongolia, yote ikipigwa nchini Azerbaijan, michezo hiyo ikiandaliwa na Shirikisho la Soka Duniani, Fifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema wachezaji wanaocheza soka la ndani ambao wameitwa kwenye kikosi hicho wameingia kambini jana na leo wameondoka.

Alisema kwa wanaocheza soka la kulipwa watajiunga na timu hiyo nchini Azerbaijan wakitoka katika mataifa ambayo wanacheza.

“Wachezaji wote ambao wameitwa katika kikosi wataungana na wenzao leo baada ya kuwasili nchini humo, watacheza mechi hizo mbili kwa mujibu wa Kalenda ya FIFA Series baada ya mechi ya mwisho dhidi ya Mongolia wachezaji watarejea.

“Tumezingatia muda kwa wachezaji ambao wana majukumu ya kimataifa ikiwamo kwa wale wa Simba na Yanga ambao wanamichezo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika,“ alisema Ndimbo.

Kikosi cha wachezaji 23 ni makipa, Aishi Manula (Simba), Aboutwaleeb Mshery (Yanga) na Kwesi Kawawa (Syrianska FC - Sweden). Mabeki ni Bakari Mwamnyeto na Ibrahim Bacca (Yanga).

Lusajo Mwaikenda (Azam FC), Haji Mnoga (Aldershot Town - Uingereza, Mohammed Hussein na Kennedy Juma (Simba), Novatus Miroshi (Shakhtar Donestsk - Ukraine) na Miano Danilo (Villena

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >